Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
Jumapili Machi 28, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580533

UK. 20



**TID maombi yako tu yanatosha**

## MAKALA MAALUM:
### Hapa ndipo kilimo kinapokwamia

KILIMO ni sekta kubwa na muhimu kwa maendeleo kutokana na mchango wake katika uchumi wa



UKURASA 5

## MAISHA
Machi 28, 2021 Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*




**HARUSI**
Ukurasa 12



Ukurasa 15
**MAISHA NI NYUMBA**
NG`ARISHA USO WA MBELE WA NYUMBA

**Fahamu faida ya samaki**
Ukurasa 14





**MATITI MAKUBWA**
**Mwonekano unaopendwa na watu wengi**

UKURASA 9

# Mambo haya 12 turufu ya kumpaisha Rais Samia

UKURASA 4



## YALIYOMO
UKURASA WA 3

**DARAJA LAKATA MAWASILIANO**
WANANCHI wa Kijiji cha Mgowelo, Kata ya Nyanzwa wilayani Kilolo mkoani Iringa ...

# Familia ya Nyerere yazuru Chato, yatoa ujumbe mzito

UKURASA 2

## Makada 25 wachuana kumrithi Nditiye

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YATAMBA KUKWEPA VIUNZI UK. 24

MAONI, KATUNI UK.6

# Dar wabainisha matarajio yao kwa Rais Samia

Na Maulid Mmbaga

BAADHI ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa na wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, wamebainisha matarajio yao kwa uongozi wa Rais mpya, Samia Suluhu Hassan, katika ustawi wa demokrasia na maendeleo ya taifa.

Mmoja wa wachambuzi hao, Said Miraji, alisema ustawi wa demokrasia nchini utachangia maendeleo kwa kuwa watu watakuwa na uhuru wa kutoa mawazo na kushiriki katika masuala mbalimbali na hata kukosoa pale patakapokuwa na shida.

"Kila jambo lina faida na hasara, lakini serikali ikifungua milango ya kidemokrasia na viongozi wakasimamia vizuri, faida itakuwa kubwa zaidi kuliko hasara na watu watakuwa na mapenzi baina yao," alisema.

Abdukarim Atiki, mchambuzi wa masuala ya kisiasa nchini, alisema Hayati Dk. John Magufuli alipinga utaratibu wa walionacho kuwanyonya wasionacho.

Mchambuzi huyo alisema si Tanzania tu ambayo inapingana kisiasa na aliziorodhesha nchi zingine zinazotumia mfumo huo zikiwamo Venezuela na Quba, akibainisha kuwa msimamo ulioanzishwa na aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Julius Nyerere katika kudai kilicho chao, uendelezwe.

"Huo ndiyo msimamo aliotuachia Rais Nyerere kwamba ni lazima utu na heshima ya mwanadamu iwe mstari wa mbele kwa ajili ya Watanzania na maslahi ya taifa kwa ujumla," alisema.

Batuli Adam, mkazi wa Dar es Salaam, alisema Watanzania katika kipindi hiki wanatakiwa kushikamana na kuwa na ushirikiano katika kuhakikisha taifa linaendelea kutoka pale Hayati Rais Magufuli alipoishia na kupiga hatua zaidi.

"Tuna matumaini na Rais Samia katika kutuongoza na kusimamia vizuri Watanzania, na kutokana na umahiri wake katika utendaji, sina shaka atatuletea maendeleo zaidi katika taifa letu," alisema.

Hamza Juma, mkazi mwingine wa mkoa huo, alisema kwa wakati huu serikali inapaswa kuangalia katiba na kutafakari mwanzo mpya wa kuanza nao ili kuwasaidia viongozi na wananchi kwa ujumla.

# Familia ya Nyerere yatinga Chato

**Na Mwandishi Wetu,** CHATO

FAMILIA ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, imefika wilayani Chato mkoani Geita nyumbani kwa Hayati Rais John Magufuli kumpa pole mjane Janeth Magufuli kutokana na kufiwa na mume wake huyo.

Dk. Magufuli, Rais wa Tano wa Tanzania, alifariki dunia Machi 17, mwaka huu katika Hospitali ya Mzena mkoani Dar es Salaam na mwili wake kuzikwa juzi wilayani Chato. Akizungumza kwa niaba ya familia ya Baba wa Taifa, Msemaji wa Familia hiyo kutoka Ukoo wa Burito, Chifu Japhet Wanzagi, alisema wameamua kwenda Chato kutoa salamu za rambirambi kwa Mama Janeth kutokana na kuguswa na msiba huo.

Chifu Wanzagi alisema salamu hizo za rambirambi walizotoa zimeambatana na ng'ombe dume mmoja kama sehemu ya kumtia faraja mjane wa marehemu kulingana na mila na desturi za kabila la wazanaki linaloelekeza msiba ukitokea, sehemu za utawala ni wajibu kutoa ng'ombe dume.

"Tumekuja kuwakilisha salamu za ukoo. Tunashukuru kwamba baada ya mazishi, tumepata nafasi kufika nyumbani kuonana na mjane, Mama Janeth na familia. Tumekuja kuhani na tumetoa ng'ombe mmoja dume kama rambirambi yetu. "Hayati Dk.Magufuli tutamkumbuka kwa mengi, amefanya kazi nzuri na kubwa katika taifa. Neno la Mungu linasema 'kuwakumbuka wenye haki ni baraka'," alisema Chifu Wanzagi.

Vilevile, Chifu wanzagi aliwasilisha salamu za pole kwa Mama Janeth Magufuli zilizotumwa na Mama Maria Nyerere ambaye amemtakia heri na nguvu ya ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu anachopitia.

Aliwasilisha salamu hizo kwa Mama Janeth Magufuli akiwa amefuatana na Daisy Nyerere, Neema Nyerere, Nashom Jirabi na Madaraka Nyerere, ambao wote walikiri kuguswa kwa dhati na msiba uliotokea.

Akishukuru baada ya kupokea salamu hizo za rambirambi, Mama Janeth Magufuli, akiwa bado katika hali ya majonzi, alieleza kufarijika baada ya kupokea salamu hizo za rambirambi kutoka kwa Mama Maria Nyerere na familia yote ya Nyerere na kusisitiza kuwa yupo pamoja kwa maombi, sala na dua za Watanzania wote katika kipindi hiki kigumu.

"Msalimieni sana Mama Maria Nyerere, mfikishieni salamu, mwambieni ninampenda, ni mama yangu, tuko pamoja, asante kwa zawadi nzuri aliyonipa.

"Mama huyu alikuwa na upendo kwenye familia yangu na mume wangu pia. Mungu ambariki sana na nyie mliokuja Mungu awabariki, mmetumwa kama wawakilishi," alisema.



Mkazi wa Kijiji cha Panga la Muingereza, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, akiandaa tanuli la kuchoma mkaa juzi, kwaajili ya kuuza ili ajipatie riziki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM wapigana vikumbo uchaguzi mdogo

**Na Deogratius Nsokolo,** KIBONDO

WANACHAMA 25 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamechukua fomu kuwania ubunge katika Jimbo la Muhambwe wilayani Kibondo mkoani Kigoma.

Jimbo hilo liko wazi baada ya aliyekuwa mbunge wake na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atashasta Nditiye, kufariki dunia Februari 12, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Katibu wa CCM katika wilaya hiyo, miongoni mwa waliochukua fomu ni mbunge wa zamani wa jimbo hilo na aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Felix Kijiko, mfanyabiashara Jamal Tamim na Daktari Florence Samizi.

Wengine ni pamoja na Dickson Bidebeli, Dk. Donasiana Stephano, Shukuru Gwamagobe, Filbert Nisuzi, Nduhilibusa Mapigano, Dk. Joseph Tutuba, Juhudi Ngarama, Zabron Wailalo, Nyinisaeli Gwamagobe na mwandishi wa habari, Prosper Kwigize.

Jimbo hilo pia limewavutia David Ntezidyo, Hassan Mgutta, Dk. Chrispine Shami, Fredrick Rulagilije, Regina Kayabu, Dyagombwa Ntimba, Amina Kanyogoto, Dk. Arkado Barakabise, Philipa Mturano, Richard Makera, Adrian Sabudema na Baraka Budogo.

Uchukuaji wa ndani ya CCM kuwania jimbo hilo ulianza Machi 24 mwaka huu na kukamilika Machi 25 na wote waliochukua fomu, walifanikiwa kuzirejesha.

Kaimu Katibu wa CCM Wilaya ya Kibondo, Tausi Feruzi, alisema kuwa baada ya kukamilika kwa uchukuaji fomu na kuzirudisha, upigaji kura za maoni ulitarajiwa kufanyika jana ili ya kumpata mwanachama atakayepeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika Mei 2, mwaka huu.

Alisema kuwa wagombea wote wamepewa maelekezo ya kufanya ikiwa ni pamoja na kujiepusha na vitendo vya rushwa na atakayebainika kukiuka taratibu, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupitia kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dk. Wilson Mahera, imeshatoa ratiba ya uchaguzi ikionyesha kuwa wagombea kupitia vyama mbalimbali vya siasa watachukua fomu kwa msimamizi wa uchaguzi Machi 28 hadi Aprili 3 mwaka huu.

Vilevile, siku hiyo ya Aprili 3 itakuwa ndiyo siku ya uteuzi wa wagombea na kampeni zitaanza Aprili 4 hadi Mei Mosi na uchaguzi utafanyika Mei 2.

Nditiye alifariki dunia Februari 12 kwa ajali ya gari mjini Dodoma.

## HABARI KITAIFA



Meneja wa kampuni ya Lucky Well ya China, Feng Hun Chen (wa kulia), akikabidhi msaada wa vyakula mbalimbali yakiwamo mafuta ya kupikia kwa Mwasisi wa vituo vya kulelea watoto yatima vya Umra, Rahma Juma, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kuwafariji katika kipindi cha maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NEC yapuliza kipenga uchaguzi wa ubunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza ratiba ya uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Muhambwe mkoani Kigoma baada ya kupokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge kuwa kiti hicho kiko wazi.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na NEC na kutiwa saini na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume hiyo, Dk. Willson Mahera, ilibainisha kuwa uchaguzi huo umepangwa kufanyika Mei 2 mwaka huu.

"Tume ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ameitaarifu tume uwapo wa nafasi wazi ya kiti cha ubunge katika Jimbo la Muhambwe, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma," Dk. Mahera alisema katika taarifa yake hiyo. Alisema kuwa kwa kuzingatia kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ambacho kinaitaka tume kujaza nafasi ya kiti cha ubunge katika kipindi kisichopungua siku 20 na kisichozidi siku 50 tangu kutokea kwa sababu iliyoacha nafasi wazi ya kiti hicho, tume imeamua kutangaza mchakato wa uchaguzi huo.

"Kutokana na matakwa hayo ya kisheria, tume inautaarifu umma kuwa Jimbo la Muhambwe liko wazi na uteuzi wa wagombea utafanyika Aprili 3, mwaka huu ambayo ni siku ya 49 tangu kutokea kwa kifo hicho (cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo)," alisema.

Dk. Mahera alisema maandalizi kwa ajili ya uchaguzi huo yameshafanyika na kazi ya utoaji fomu za uchaguzi kwa wagombea inaanza leo hadi Aprili 3, huku uteuzi wa wagombea watakaowania nafasi hiyo ukitarajiwa kufanyika Aprili 3, mwaka huu.

Dk. Mahera alisema kampeni za uchaguzi huo zitaanza Aprili 3 mwaka huu na zitafikia ukomo wake Mei Mosi mwaka huu na uchaguzi kufanyika Mei 2 mwaka huu.

Alisema tayari tume imekwishavitaarifu vyama vya siasa kwa njia ya barua juu ya kuwapo kwa uchaguzi huo mdogo na inavikumbusha kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, miongozo na maelekezo ya tume wakati wote wa kipindi cha uchaguzi.

Dk. Mahera alitumia fursa hiyo kutoa salamu za pole kwa viongozi wa serikali, familia na Watanzania wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli. "Tume inatoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, familia ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Chama Cha Mapinduzi na Watanzania wote kwa ujumla," alisema Dk. Mahera.

Uchaguzi katika Jimbo la Muhambwe unafanyika baada ya Mbunge wake (CCM), Atashasta Nditiye kufariki dunia Februari 12 mwaka huu akiwa Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma alikokuwa akipatiwa matibabu baada ya kupata ajali ya gari eneo la Nanenane jijini humo Februari 11, mwaka huu.

# Mamilioni kung'arisha barabara za TARURA

**Na Stevie Chindiye,** SONGEA

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, imeidhinishiwa Sh. milioni 789 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Meneja wa TARURA katika Halmashauri hiyo, John Ambrosi, alisema jana kuwa halmashauri hiyo ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,057.

Kati yake, barabara za lami ni kilometa 13.77, kilometa 250 ni barabara za changarawe na barabara za udongo ni zaidi ya kilometa 700.

Alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21, TARURA wamepanga kutekeleza mikataba sita ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 1.396.

Kati yake, Sh. milioni 701 ni kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Muhukuru na fedha inayobakia ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Meneja huyo alisema kuwa katika mwaka wa fedha wa 2019/20, TARURA ilikuwa na mradi wa ujenzi wa daraja la Muhukuru ambao unatekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21.

Alisema utekeleza wa miradi hiyo ulianza Agosti mwaka jana na hadi kufikia Novemba, miradi minne kati ya sita ilikuwa imetekelezwa na hadi kufikia Juni mwaka huu, miradi yote inatarajiwa kukamilika kwa asilimia 100.

Licha ya jitihada zinazofanywa na wakala huo kuimarisha barabara, madaraja na vivuko, meneja huyo alisema kumekuwa na vikwazo mbalimbali vinazoathiri miundombinu ikiwamo magari yenye uzito mkubwa na mvua za masika.

Baadhi ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, wakiwamo wa Kijiji cha Litowa, waliusifu wakala huo kwa kuwasaidia kukarabati kivuko kinachounganisha kitongoji cha Goliama na Litowa.

Hata hivyo, Christina Njovu na Egno Mwalongo, walisema kivuko hicho kimekuwa kero kwao kwa sababu magari hayawezi kuvuka pia kinahatarisha usalama wao, hivyo wanaiomba serikali kuwajengea daraja la kudumu.

Akizungumzia kero ya vivuko hivyo, Meneja wa TARURA, Ambrosi, alisema wanatambua shida hiyo lakini kwa sasa bado hawajapata fedha ya kujenga daraja la kudumu.

Alisema TARURA imejenga kivuko cha mbao chenye urefu wa kilometa 21 na wamekuwa wanakifanyia matengenezo ya mara kwa

# Daraja lakata mawasiliano

**Na Halfani Chusi**

WANANCHI wa Kijiji cha Mgowelo, Kata ya Nyanzwa wilayani Kilolo mkoani Iringa, wameiomba serikali kuharakisha ujenzi wa daraja lililobomoka kwa kuwa ni tegemeo katika kuunganisha vijiji wanavyopakana navyo.

Akizungumza na Nipashe jana, mkazi wa kijiji hicho, Jimi Mtarula, alisema daraja hilo ni kiunganishi cha kijiji chao na Kijiji cha Mtandika ambako wamekuwa wakitegemeana katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mtarula alisema tangu daraja hilo libomoke, wananchi wamekuwa wakilazimika kupanda gari hadi eneo la daraja kisha kuvuka kwa miguu na kuchukua gari lingine upande wa pili.

Diwani wa Nyanzwa, Katili Mgwale, alisema daraja hilo lilibomoka takriban siku tatu zilizopita na kusababisha wananchi kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

"Baada ya kupokea taarifa kutoka Serikali ya Kijiji cha Mgowelo, nilikwenda eneo la tukio na kukuta daraja limebomoka na abiria wameshindwa kuendelea na safari ndipo nilipowasiliana na uongozi wa Wilaya ya Kilolo," alisema.

Alisema wataalamu wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), walifika eneo hilo na kupiga picha na kuahidi kurudi kushughulikia tatizo hilo.

"Kwa sasa (jana) ninakwenda eneo la tukio kujadiliana na wananchi wa Kijiji cha Mgowelo, ambao ndiyo waathirika, kutengeneza njia ya dharura pembeni itakayotumika kwa muda wakati wakiwa wakisubiri matengenezo ya daraja," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Bakari Mtarula, alisema tangu daraja hilo libomoke, shughuli za kimaendeleo zimekwama kwa kiasi kikubwa.

"Wananchi wa Mgowelo na Nyanzwa wanategemea daraja hili kupitisha mizigo kutoka shambani kuipeleka mjini, shughuli nyingi kwa sasa zimesimama," alisema.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Kumbuka Malenda, aliwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati wakiendelea kushughulikia tatizo hilo.

# Mambo haya 12 kumpaisha Samia

Na Mwandishi Wetu

TANZANIA iko katika enzi mpya ya uongozi. Enzi hiyo ni ya Samia Suluhu Hassan, Rais wa kwanza mwanamke katika ukanda wa Afrika Mashariki, ambaye ameshika kijiti cha uongozi baada ya kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17 mwaka huu.

Rais Samia ambaye kabla ya hapo alikuwa Makamu wa Rais, alishika rasmi uongozi Machi 19 baada ya kula kiapo. Kwa kushika wadhifa huo, Samia ameandika rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Tanzania. Kabla ya hapo, alikuwa na rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Makamu wa Rais tangu kuasisiwa kwa taifa la Tanzania.

Tangu ashike wadhifa huo, kumekuwa na mitazamo tofauti kama anaweza 'kutosha' katika 'viatu' vya mtangulizi wake, akiwa Rais wa Sita wa Tanzania. Hiyo yote, kwa sehemu kubwa, inatokana na ukweli kwamba haijawahi kutokea katika historia ya Tanzania.

Lakini wakati wa mazishi ya kitaifa ya Rais Magufuli yaliyofanyika wiki hii katika Uwaja wa Jamhuri jijini Dodoma, aliwatoa hofu Watanzania alivyoeleza kwa kinagaubaga kwamba anatosha.

"Kwa wale ambao wana mashaka, 'mwanamke huyu ataweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?' ninataka niwaambie aliyesimama hapa ni Rais... ninataka nirudie, aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye maumbile yake ni mwanamke," alisema.



Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MAMBO YA KUMPAISHA**

Katika kutekeleza majukumu yake na kuthibitisha kuwa anatosha, yako mambo mengi ambayo yatampaisha na kuonyesha anaweza. Miongoni mwa mambo hayo ni; -

**DEMOKRASIA**

Katika ngwe ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano, ilidaiwa kuwa kulikuwa na kuminywa kwa demokrasia na uhuru wa kukusanyika, hatua ambayo iliwafanya Watanzania kushindwa kutoa madukuduku yao au kuvijenga vyama vyao.

Kutokana na hali hiyo, wapinzani wana kiu na matamanio ya kuona kama Rais Samia anaweza kulegeza masharti na kuruhusu wapinzani kukutana na kufanya mikutano.

**BUNGE 'LIVE'**

Tangu kuanza kwa serikali ya awamu ya tano, Watanzania walikosa uhondo wa kushuhudia moja kwa moja mijadala ya mikutano ya Bunge na badala yake kilichokuwa kikionyeshwa ni Hotuba ya Bajeti na Maswali na Majibu.

Hivi sasa mjadala uliopo ni je, maonyesho hayo mubashara ya bunge yatarejeshwa ili kuona mijadala motomoto ikiendelea katika chombo hicho cha kutunga sheria?

**NYONGEZA MISHAHARA**

Hili ni suala ambao limekuwa likigonga katika vichwa vya wengi kutokana na ukweli kwamba tangu mwaka wa fedha wa 2015/16 mishahara kwa watumishi wa umma haijawahi kupandishwa. Sababu kubwa ambayo serikali ilikuwa ikitoa ni kudhibiti mfumuko wa bei.

Hata hivyo, wafanyakazi hasa watumishi wa umma, mashirika na taasisi za serikali, wana hamu ya kuona kama ukimya huo wa kutopandishwa mishahara utavunjwa.

Mei Mosi, mwaka huu, ambayo ni Sikukuu ya Wafanyakazi, itafanyika kwa mara ya kwanza Samia akiwa Rais, hivyo macho na masikio ya Watanzania ni kutaka kusikia kama atavunja ukimya na wafanyakazi kuwa na kicheko.

**KIKOKOTOO**

Mwaka 2018, kuliibuka mjadala mkali nchini kuhusu ukokotoaji wa mafao ya wastaafu baada ya serikali kuja na marekebisho ya sheria yaliyolenga kubadili utaratibu wa wastaafu kupewa asilimia 75 ya mafao yao kisha asilimia 25 inayobaki kupewa kidogo kidogo kila mwezi na kuwa kinyume chake.

Hayati Rais Magufuli aliingilia kati suala hilo na kuagiza kikokotoo kipya kianze kutumika mwaka 2023. Kitakachompaisha Rais Samia katika hili ni kuendelea na kikokotoo cha zamani.

**MIRADI MIKUBWA**

Katika serikali ya awamu ya tano, kumekuwa na kasi ya utekelezaji wa miradi mikubwa katika sekta za afya, masoko, maji, umeme, reli ya kisasa, ujenzi wa barabara na madaraja ambayo inagharimu mabilioni ya shilingi.

Miradi hiyo imeifanya serikali ya awamu ya tano kupata sifa kubwa kwa kuwa imesaidia kutatua matatizo yaliyokuwa yakiwakabili wananchi. Kama Rais samia alivyosema baada ya kula kiapo kuwa "hakitaharibika kitu", Watanzania wana imani kuwa kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo itakuwa kama mwanzo au zaidi.

**RUSHWA NA UFISADI**

Serikali ya awamu ya tano imekuwa ikipambana na vitendo vya rushwa na ufisadi ambavyo kwa muda mrefu vilirudisha nyuma maendeleo ya nchi. Katika kutekeleza hilo, serikali ilianzisha Mahakama ya Uhujumu Uchumi, maarufu kama Mahakama ya Mafisadi.

Watu wengi waliotuhumiwa na kuhusika na vitendo hivyo wamefikishwa mahakamani na wengine kuchukuliwa hatua. Ni imani kwamba kasi hiyo itaendelea katika uongozi wa Rais Samia.

**ULINZI, USALAMA**

Vitendo vya ujambazi na ujangili katika hifadhi za taifa vilikithiri kwa muda mrefu. Lakini katika uongozi wa awamu ya tano, vitendo hivyo vimepungua kwa kiasi kikubwa na serikali kupata sifa kemkem.

Ni imani kwamba hali hiyo ya kuimarishwa kwa ulinzi na usalama itaendelezwa katika uongozi wa Rais Samia na Tanzania kuendelea kuwa shwari kwa maana ya wananchi, mali zao na maliasili za taifa.

**ELIMU**

Sekta ya elimu imepiga hatua kubwa ndani ya uongozi wa Dk. Magufuli na Rais Samia katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ongezeko la wanafunzi elimu ya awali hadi chuo kikuu, kuongezeka kwa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu

Ni dhahiri kwamba chini ya uongozi wa Samia, sekta hiyo ambayo ni tegemeo la maendeleo ya taifa, itazidi kupewa kipaumbele kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kama ambavyo imekuwa ikitekelezwa.

**MAKUSANYO MAPATO**

Msingi mkuu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni makusanyo ya maopato ya kodi na yasiyo ya kodi. Ndani ya miaka mitano, kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato, hivyo kuifanya serikali kupata sifa kutokana na kazi hiyo.

Mwaka 2015 wakati Dk. Magufuli na Rais Samia wanaingia madarakani, wastani wa makusanyo ya mapato ulikuwa Sh. bilioni 850 kwa mwezi lakini hadi mwaka huu uliongezeka hadi kufikia wastani wa Sh. trilioni 1.4.

Kasi hiyo ya ukusanyaji wa mapato, ni dhahiri kwamba itaongezwa ili kutimiza ndito za kufikia wastani wa Sh. trilioni mbili au zaidi kwa mwezi.

**NISHATI**

Tanzania hivi sasa iko katika mkakati wa kufikia uchumi wa kati ambao unabebwa na dhima ya maendeleo ya viwanda.

Ili kufikia azma hiyo, suala la nishati hasa umeme wa uhakika ni la muhimu. Katika kutambua hilo, pamoja na mambo mengine, kuna ujenzi wa mradi wa umeme katika Bwawa la Nyerere kwenye Mto Rufiji.

Kukamilika kwa mradi huo, kutawezesha kupatikana kwa megawati 2,115 ambazo zitawezesha Tanzania kuwa na umeme wa ziada ambao utachochea maendeleo ya viwanda na hata ziada kuuzwa nje.

Kasi hiyo pamoja na utafutaji wa vyanzo vingine vya nishati itaendelea chini ya Rais Samia, hivyo kuleta mapinduzi ya viwanda.

**VYOMBO VYA HABARI**

Kilio kikubwa kwa wanahabari kimekuwa kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari. Kilio hicho kiliambatana pia na madai ya kukosa matangazo kutoka idara na taasisi za serikali, hivyo kulazimu baadhi ya vyombo vya habari kufungwa kutokana na ukata.

Swali linalotanda katika tasnia hiyo ni, je, hali hiyo itaendelea au italegezwa?

Sambamba na mambo hayo, pia Watanzania wana kiu ya kuona kama nidhamu katika utumishi wa umma itaendelezwa katika kasi ile ile pamoja na ujenzi wa masoko katika maeneo mbalimbali ambapo kumekuwa na ujenzi wa miundombinu ya kisasa na wafanyabiashara wananufaika nayo.

MAKALA MAALUM

# Hapa ndipo kilimo kinapokwamia

## ■Ripoti yaanika pia vikwazo lukuki katika Sekta ya Elimu

Na Mwandishi Wetu

KILIMO ni sekta kubwa na muhimu kwa maendeleo kutokana na mchango wake katika uchumi wa nchi. Takwimu za Wizara ya Kilimo zinabainisha kuwa mwaka 2017, sekta hiyo ilitoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 65.5, huku ikichangia asilimia 28.7 ya Pato la Taifa.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta hiyo, imepanga kubadilisha kilimo kutoka kuwa cha kujikimu na kuwa cha kibiashara.

Mabadiliko hayo yanafanyika kwa kuzingatia malengo ya kitaifa yaliyowekwa hususan yaliyoko kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo unaoweka mkazo katika mapinduzi ya viwanda, unaoitambua Sekta ya Kilimo kama mhimili imara utakaowezesha upatikanaji wa malighafi za viwanda.

Ikumbukwe kuwa miongozo hiyo ya kitaifa pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 na Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013, inatekelezwa na Wizara ya Kilimo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDPII).

Licha ya kuwapo kwa miongozo hiyo, Sekta ya Kilimo nchini bado inakabiliwa na vikwazo kadhaa, kikubwa kikiwa ni upungufu katika kutenga na kutoa fedha za bajeti ya sekta hiyo muhimu.

Taasisi ya WAJIBU kupitia ufadhili wa Foundation for Civil Society (FCS) imefanya uchambuzi wa Sekta ya Kilimo, ikiangazia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2019/20.



Uchambuzi wa WAJIBU unaonyesha kuwa bajeti ya kilimo imekuwa ikishuka kila mwaka ikitoka asilimia 0.71 ya bajeti yote ya serikali mwaka 2016/17 hadi asilimia 0.63 kwa mwaka 2018/18.

Hali hiyo ni kinyume cha makubaliano ya kimataifa ya Maputo na Malabo yanayozitaka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya bajeti zake kwa Sekta ya Kilimo.

"Mwaka 2016/17, bajeti ya Wizara ya Kilimo ilikuwa Sh. bilioni 629, mwaka uliofuata Sh. bilioni 618 na mwaka 2018/19 ilikuwa Sh. bilioni 340. Kutotenga bajeti kwa asilimia 10 kunapunguza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kama kipaumbele cha taifa," Meneja Fedha na Utawala wa WAJIBU, Jackson Mmary anasema.

Mmary anabainisha kuwa licha ya bajeti ya kilimo kutokufikia asilimia 10 ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2018/19, serikali haikutoa asilimia 41 ya fedha za miradi ya maendeleo kwenye miradi ya kilimo.

Anaendelea kubainisha kuwa kwenye mradi wa uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT-CTF), serikali haikutoa asilimia 84 ya bajeti yake.

"Kushindwa kutoa fedha hizo kunapunguza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya kilimo nchini. Hivyo basi, WAJIBU inashauri Asasi za Kirai (AZAKI) kwa kushirikiana na halmashauri, ziendelee kufanya ushawishi juu ya uongezwaji na utolewaji wa bajeti ya kilimo kama matamko ya kitaifa na kimataifa yanavyotaka," anashauri.

Katika ripoti yake ya mwaka 2018/19, CAG alibaini malipo yasiyokubaliwa ya Sh. milioni 53.8 kwenye mradi wa upanuzi wa uzalishaji wa mpunga.

CAG pia alibaini serikali kutochangia Sh. milioni 712.95 (asilimia 89) ya gharama za miradi kulingana na makubaliano na washirika wa maendeleo katika mradi wa upanuzi wa mpunga.

Vilevile, ripoti yake hiyo ilibaini bakaa za akaunti za washirika ambazo hazikutumiwa kwa muda kiasi cha Dola za Marekani 4,275,792.12.

"Kutokana na upungufu uliobainishwa na CAG, WAJIBU inashauri AZAKI husika kwa kushirikiana na halmashauri kufuatilia upungufu huo," taasisi hiyo inashauri katika ripoti yake ya uchambuzi.



**SEKTA YA ELIMU**

Uchambuzi wa WAJIBU ulirejea taarifa ya Takwimu za Elimu Msingi Tanzania (BEST 2018) zinazobainisha kuwa matundu ya vyoo shuleni yaliongezeka kutoka 190,674 mwaka 2016/17 hadi kufikia 197,741, sawa na uwiano wa 1:56.

Vilevile, vyumba vya madarasa viliongezeka kutoka 119,647 mwaka 2016/17 hadi kufikia 122,487, sawa na uwiano wa 1:81.

Katika uchambuzi wake, WAJIBU inabainisha kuwa halmashauri saba kati ya 14 zilizokaguliwa, hazikuwa zimefikia uwiano uliowekwa na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) unaotaka tundu moja la choo kuhudumia wanafunzi 56.

Halmashauri hizo ni za Jiji la Mbeya, Wilaya za Liwale, Sumbawanga, Gairo, Handeni, Malinyi na Mji wa Kahama huku halmashauri za Jiji la Mbeya, Manispaa ya Bukoba, Wilaya za Handeni, Milinyi, Gairo, Sumbawanga na Miji ya Kahama zikishindwa kufikia uwiano uliowekwa na mpango huo unaotaka darasa moja kuhudumia wanafunzi 75.

"Kutokana na baadhi ya Halmashauri kushindwa kufikia uwiano wa madarasa na matundu ya vyoo kama ilivyoelezwa kwenye muongozo, WAJIBU inashauri AZAKI zinazofanya ufuatiliaji wa mradi huu, zifanye ushawishi katika ngazi ya halmashauri ili shule hizo zitekeleze mwongozo husika.

"Katika kufanya ufuatiliaji, AZAKI ziangalie kiwango na ubora uliokusudiwa, thamani ya fedha, vitendo na viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu na kama wananchi wananufaika ama wanapata huduma stahiki kulingana na malengo ya miradi hiyo," taasisi hiyo inashauri.

Taasisi hiyo pia inarejea ripoti ya CAG kwa mwaka 2018/19, iliyobaini Sh. bilioni 2.9, fedha za ruzuku kwa shule za sekondari na msingi, hazikutolewa.

"Tathmini iliyofanywa na CAG kuhusu utekelezaji wa elimu bila malipo kwa mwaka fedha 2018/19 katika halmashauri 42, inaonyesha Sh. bilioni 2.9, sawa na asilimia 24 ya kiasi kilichokadiriwa, hazikutolewa.

"Halmashauri mbili kati ya 14 zilizokaguliwa, hazikupokea fedha za ruzuku ya elimu bila malipo Sh. milioni 317.11 kwa shule za msingi na sekondari.

"Utoaji wa fedha pungufu, unazifanya shule kushindwa kununua vifaa muhimu vya elimu kama vifaa vya kufundishia, vifaa vya maabara na kemikali pamoja na marekebisho madogo madogo ya miundombinu ya shule.

"Hii huathiri ubora wa mazingira ya kufundishia pamoja na uwezo wa wanafunzi kujifunza. WAJIBU inashauri AZAKI husika kuziwezesha Kamati za Elimu na Kamati za PETS/SAM kufanya ushawishi kwa serikali juu ya utoaji wa fedha zinazokuwa zimepangwa katika kuleta ufanisi ndani ya sekta ya elimu.

"Vilevile, kamati hizi zifanye ufuatiliaji wa fedha ambazo zimepokewa katika ngazi ya shule husika, ili kuhakikisha fedha hizo zinaboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia," taasisi hiyo inashauri.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Njia pekee kwa Watanzania kumuenzi JPM ni kufanya kazi

**WATANZANIA** bado wako kwenye majonzi kutokana na kuondokewa na kipenzi chao, Rais wa Tano, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Kutokana na kifo hicho, Rais Samia Suluhu Hassan, aliyechukua hatamu za uongozi baada ya kifo cha kiongozi huyo, aliyejulikana maarufu kama JPM, alitangaza maombolezo kwa siku 21 huku bendera zikipepea nusu mlingoni.

Hatimaye Dk. Magufuli juzi alipumzishwa katika nyumba yake ya milele kijijini kwao, Mlimani, Chato mkoani Geita katika makaburi ya familia. Hatutamwona tena mwanamapinduzi huyo na shujaa wa Afrika, aliyelitumikia taifa kwa moyo wa uzalendo na kutumia muda mwingi kuwatumikia Watanzania.

Dk. Magufuli, aliyeitwa majina mbalimbali kama vile 'tingatinga', jembe, chuma na kifaa, yote hayo kuonyesha uchapakazi wake, amewaliza Watanzania, wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika nzima. Hiyo inadhihirishwa kutokana na marais mbalimbali wa Afrika walivyohudhuria mazishi yake na wengine kutuma salamu kutokana na kifo chake.

Kutokana na misimamo yake, falsafa zake na kukiishi kile anachokiamini, katika kipindi cha takriban miaka mitano na miezi minne, ameacha alama ambayo itakumbukwa na vizazi vya sasa na vijavyo. Mambo atakayokumbukwa nayo ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, mradi wa umeme katika Mto Rufiji maarufu kama bwawa la Mwalimu Nyerere, Daraja la Juu la Kijazi, daraja la Mfugale na kufufua Shirika la Ndege la Tanzania.

Hayo ni yale yanayoonekana dhahiri lakini pia amefanya mambo makubwa katika ujenzi wa barabara na madaraja, kuboredha sekta ya afya kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, rufani za mikoa na za kanda. Kadhalika ameboresha elimu kwa kuongeza mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ongezeko la udahili elimu ya juu, ujenzi wa miundombinu shule za sekondari na za msingi pamoja na kutoa elimu bure.


Matokeo ya hayo aliyoyafanya ikiwa ni pamoja na kuongeza mapato kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 alipoingia madarakani mwaka 2015 hadi Sh. trilioni 1.3, kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma na kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati, ni kielelezo kwamba anastahili kukumbukwa na kuenziwa.

Lakini swali la kujiuliza aenziwe kwa manna gani? Jibu liko wazi kwamba njia pekee ya kumuenzi Mtanzania huyo halisi, aliyejitolea kuitoa Tanzania katika lindi la umaskini ni kufanya kazi kwa juhudi na maarifa.

Watanzania bado wana imani na Rais Samia ambaye wakati wa uongozi wa Dk. Magufuli alikuwa makamu wa Rais na kuahidi kuwa hakuna kitakachoharibika, hivyo aungwe mkono kuipeleka Tanzania katika hatua ya juu zaidi ya maendeleo.

Iwapo kila Mtanzania atasimama na kufanya kazi kwa bidii zake na kwa nafasi aliyonayo, Tanzania itafikia kipeo cha juu cha maendeleo. Hiyo ndiyo itakuwa njia pekee ya kumuenzi kipenzi wetu Hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Watanzania tumuenzi Magufuli kwa kuhimiza uzalendo miongoni mwetu

**LEO** ni siku ya 12 tangu Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, afariki dunia na kuzikwa nyumbani kwao Chato mkoani Geita. Bado Watanzania wanaendelea kuomboleza msiba huo mzito.

Kipindi cha miaka mitano na miezi michache ambayo amekaa madarakani, alijipambanua kuwa ni mtu anayetamani kuiona Tanzania inapiga hatua na kufika mbali katika maendeleo.

Aliamini kwamba ili Tanzania iwe na maendeleo, wananchi hawana budi kuwa wazalendo na kuitakia mema nchi yao badala ya kukaa na kuizungumzia vibaya ndani na nje.

Neno uzalendo lina herufi nane lakini lenye maana pana ambayo Dk. Magufuli alikuwa akimaanisha na kulirudia mara kwa mara kwenye vikao na mikutano mbalimbali hapa nchini.

Kwa mfano, baadhi ya watu wanasema, mtu anapoipenda nchi yake ni uzalendo, kwamba ni miongoni mwa tabia zinazochochea maendeleo yake na hata ya nchi yake kwa ujumla.

Uzalendo pia inaelezwa kuwa humsukuma mtu kuithamini na kuionea fahari nchi yake na kuitakia mema, kwamba, mzalendo ni mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa nchi yake na yuko tayari kuitetea.

Lakini pia si kila mtu ni mzalendo kwa kuwa mtu anaweza kuwa mzawa lakini asiwe mzalendo na anaweza asiwe mzawa akapata uraia na akawa mzalendo kuliko mwananchi mzawa.

Uzalendo ni moja ya mambo ambayo Dk. Magufuli alikuwa akihimiza na kuwataka Watanzania kuipenda nchi yao, ikiwa ni pamoja na kuitakia mema badala kukaa na kuisema vibaya ndani na nje.

Hata miezi ya hivi karibuni, aliagiza kuanzishwa kwa somo la historia, kwa lengo la kujenga uzalendo kwa vijana ingawa amefariki wakati mchakato wa kuanzisha somo hilo ukiendelea.

Ni vyema kumuenzi JPM kwa kuhimiza na kutanguliza uzalendo kwa nchi yetu, kwani waswahili wanasema: "mkataa kwao ni mtumwa', hivyo ingependeza kila Mtanzania kuwa mzalendo.

JPM ameacha ujenzi wa Chuo cha Uongozi cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere, ukiendelea kule Kibaha mkoani Pwani, ambacho kinatarajiwa kutoa mafunzo ya itikadi na uongozi na uzalendo kwa Watanzania.

Chuo hicho kinahusisha vyama sita vya ukombozi barani Afrika vya CCM (Tanzania) FRELIMO (Msumbiji), ANC (Afrika Kusini), SWAPO (Namibia), ZANU-PF Zimbabwe na MPLA (Angola).

Wakati huu ambao chuo kinaendelea kujengwa, ni muhimu kukumbuka lengo la JPM la kuanzisha chuo hicho ambalo pamoja na mambo mengine, ni mahali rasmi pa kuwafanya watu kuwa wazalendo wa hali ya juu.

Vilevile miezi ya hivi karibuni, JPM alitangaza kurejeshwa kwa somo la historia kama njia ya kuimarisha uzalendo miongoni mwa Watanzania, lakini amefariki wakati mchakato wa kuanzisha somo hilo ukiendelea.

Hatua hizo na nyingine nyingi alizozifanya, zinaonyesha alikuwa amedhamiria kuimarisha uzalendo miongoni mwa Watanzania, hivyo wakati huu ambao ametwaliwa na muumba wake, ni vyema matamanio yake yakaendelezwa.

Ni vyema dhana ya mtu kwao na kwa kuthamini kwao ikapewa nafasi kubwa miongoni mwetu ikiwa ni kuendeleza mema yote ambayo yalianzishwa na kusimamiwa na Dk. Magufuli.

Kila mtu anaweza kufanya tathmini kuhusu uzalendo wake kwa nchi yake na kama atabaini umeshuka, basi achukue hatua ya kubadilika ili kumuenzi JPM ambaye neno uzalendo lilikuwa likitoka kila mara mdomoni mwake.

Wapo ambao huwa wanadai kwamba uzalendo hauamasishwi, bali unakuja tu wenyewe na unasababishwa na wale tuliowakabidhi mamlaka ya nchi kuwa wazalendo kwa kila jambo na matendo.

Lakini pamoja na hayo, ni muhimu kuwahamasisha wale ambao hawaujui, ili nao wawe wazalendo kwa nchi yao, badala ya kudhani tu kwamba uzalendo unakuja wenyewe bila kuhamasishwa. Kwa kuwa aliyekuwa rais wa awamu ya tano aliona kuna tatizo kwenye uzalendo na kuamua kuhimiza Watanzania kuwa wazalendo, ni wakati sasa wa kuenzi jambo hilo kutokana na umuhimu wake kwa taifa.

Kwa kuwa mzalendo ni mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa nchi yake, kila mmoja wetu afanye sehemu yake kumuenzi JPM kwa kuthamini mchango wake katika kuhimiza uzalendo miongoni mwa Watanzania.

SAFU

AFYA

# Maajabu ya karoti kwa afya ya macho



**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya matatizo ya kiafya yanayowapata watu hivi sasa ni kutokana na kutokuzingatia kanuni za afya bora hasa ulaji wa vyakula mbalimbali kwa ajili ya kujenga na kulinda mwili.

Hatua hiyo imesababisha maradhi mbalimbali yanayotokana na upungufu wa vitamin na viinilishe ambavyo huufanya mwili kuwa na afya njema. Inawezekana baadhi ya watu wanakula milo mitatu kama inavyoshauriwa na wataalam wa afya lakini ni mlo wa namna gani?

Mtu mmoja aliwahi kumtania rafiki yake kuwa hawezi kula matunda na mboga mpaka aandikiwe na daktari! Ni ujumbe ambao unaonekana ni wa kawaida lakini unatoa msisitizo mkubwa kwa ulaji wa mboga na matunda kwa faida za kiafya.

Miongoni mwa vyakula ambavyo huenda watu wanakula kwa mazoea au kuona ni cha kawaida ni karoti. Hiki ni chakula kilicho katika jamii ya vyakula vya mizizi ambavyo vimekuwa maarufu katika familia nyingi. Kwa kiasi kikubwa hutumika kama kiungo katika mboga. Huchanganywa na viungo vingine kama vitunguu, pilipili hoho na nyanya ili kuitia mboga au kitoweo katika hali ya kupendeza.

Pamoja na matumizi hayo, karoti inaelezwa kuwa ina manufaa makubwa katika afya hasa kuimarisha nguvu ya macho (uoni).

Kama ilivyoelezwa awali, watu wengi wanaifahamu karoti kama kiungo cha mboga lakini ni zaidi ya hapo. Karoti pia tunda kwa kuwa licha ya kutumika kama kiungo katika chakula, linaweza kutafunwa kama lilivyo au kusagwa na kunywa juisi yake.

Wataalamu wa afya wanasema karoti pia ina protini kidogo na haina mafuta kama yalivyo matunda mengine. Pia ina asili ya wanga na ni chanzo kizuri cha vitamini B, C na E. Kadhalika, ina madini mbalimbali yakiwamo ya aina ya chuma.

Sambamba na hiyo, chakula hicho kina kitu kinaitwa beta - rotene ambayo kikiingia mwilini inabadilishwa na kuwa vitamini A. Pia ina kirutubisho kinachoitwa 'fiber' ambacho ni muhimu kwa kukinga kuta za utumbo.

**KINGA NA TIBA**

Karoti inasaidia kukinga na kuponya magonjwa kama macho hasa kutoona gizani au kwenye mwanga hafifu. Kutokana na umuhimu huo, inashauriwa watu kula karoti mara kwa mara ili kuimarisha afya ya macho.

Katika kusaidia kujikinga au kupunguza tatizo hilo, inashauriwa karoti itumike katika chakula ama kwa kuitafuna, kuchanganywa na viungo vingine katika mboga au kutengenezwa juisi na kuwa kinywaji. Kwa namna zote hizo, inabainishwa kwamba ni kinga na tiba mujarabu kwa macho yako.

Sambamba na faida hiyo, karoti husaidia kukinga ngozi, kupunguza tindikali inayodhuru tumboni na kukinga magonjwa yenye asili ya kansa.

Kutokana na umuhimu huo na maajabu katika afya ya mwili wa mwanadamu, kampuni mbalimbali ambazo zimekuwa zikijihusisha na masuala ya lishe na tiba, zimekuwa zikitumia karoti katika kuchanganya na mimea mingine katika utengenezaji wa virutubisho kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye matatizo ya kiafya.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Nakuandikia Rais Samia Suluhu Hassan



**Na Joseph Kulangwa**

**Hukutarajia maishani mwako kuwa Rais, ni kama wengi walivyokuwa ni majaaliwa ya Mungu hata mtu awe fulani. Nawe umefika hapo kwa majaaliwa ya Mungu wako, ambaye alikuficha siri hii hatimaye amekufunuliwa.**

RAIS Samia Suluhu Hassan, Salaam. Nakuandikia barua hii, nikitambua kuwa wewe ndiwe Rais wangu wa sita wa Tanzania.

Nakuandikia nikitambua kuwa ndiwe Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, uliyepokea mikoba kutoka kwa Dk. John Magufuli (roho yake ilazwe mahali pema peponi).

Nakuandikia kukupongeza kwa hatua hiyo ya kubeba mzigo mkubwa wa kuiongoza Tanzania, nchi iliyoachwa na Dk. Magufuli, nikiamini kuwa viatu ulivyovaa vinakutosha, na utavitumia vyema kutufikisha Watanzania kule ambako mtangulizi wako alipanga.

Umeshiriki nasi katika msiba mkubwa uliotukumba Watanzania, kupoteza kiongozi wetu akiwa madarakani na kuwa ni historia katika nchi hii, ambayo huko nyuma ilizoea kupoteza viongozi waliokwishamaliza muda wao wa uongozi.

Lakini pia nawe umeweka au kuandika historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya urais katika eneo hili la Afrika Mashariki na kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza. Naamini utaweza.

Hukutarajia maishani mwako kuwa Rais, ni kama wengi walivyokuwa ni majaaliwa ya Mungu hata mtu awe fulani. Nawe umefika hapo kwa majaaliwa ya Mungu wako, ambaye alikuficha siri hii hatimaye amekufunuliwa.

Kwa kauli yako katika baadhi ya masimulizi yako, hukuingia katika siasa, kwa sababu ya kutaka madaraka, kwani kama ulivyosema uliingia katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ili kwenda kuwazodoa mawaziri waliokuwa wanashindwa kujibu hoja za wananchi zilizopelekwa kwao na wawakilishi.

Lakini ukiwa unatarajia kuwa ukifika huko utaitumia vizuri nafasi yako kukabiliana nao kwa maslahi ya wananchi, ukajikuta unageuziwa kibao kwa kuteuliwa kuwa Waziri, hivyo ukabeba jukumu la kujibu hoja hizo, kama ulivyokuwa unatarajia kwa mawaziri waliokutangulia.

Hata siku unateuliwa kuwa mgombea mwenza wa Dk. Magufuli hukutarajia na hata ulijikuta ukitokwa machozi, si kwa furaha, bali kwa kutoamini kama nafasi hiyo ungeiweza. Lakini ukaiweza kwa uwezo mkubwa na wa kiwango cha juu, na sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongera sana Mama.

Nafasi uliyo nayo ni kubwa na ina mambo makubwa na mengi. Inaweza kuandamana na minong'ono ya hapana pale. Bahati nzuri mingine ulishaisikia na ukaikemea, kwa kusema wewe ndiwe Rais wa Tanzania katika maumbo ya kike. Ujumbe ulifika na walioelewa walikuelewa.

Watanzania wengi wameshaonyesha nia ya kukusaidia katika uongozi wako, wanataka kushirikiana nawe ili uendelee na alipoachia Dk. Magufuli, ambaye huko aliko ataendelea kukufuatilia na kuangalia unakwendaje na bila shaka atakuombea.

Hivyo sasa, Rais Samia, mema aliyoyaanza na kuyaacha Dk. Magufuli yaendeleze, usiangalie makunyanzi. Pambana na rushwa, pambana na uzembe, pamba na ufisadi. Hakikisha nidhamu ya watumishi ambayo ilishajengwa na Dk. Magufuli ambayo tofauti na zamani inafanya sasa wananchi wanahudumiwa vizuri na kwa haraka zaidi na taasisi za serikali. Dumisha hilo.

Una fursa na hiari ya kupanga safu yako unayoiamini kwamba itakusaidia kuhudumia Watanzania kwa jinsi unavyotaka na kuamini kwamba ndivyo wanavyotaka wapiga kura wako.

Kauli yako ya siku ya kuapishwa Machi 19 Ikulu, Dar es Salaam, wananchi waliielewa na bila shaka wenye nia njema wameizingatia, watakusaidia.

**Inshallah! Wasalaam!**

## KONA YA UKWELI

# Zitto sikukuelewa, nadhani majibu sasa umeyapata



Na Thobias Mwanakatwe

ALIYEKUWA Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, hatimae amezikwa kijijini kwao Mlimani, Chato mkoani Geita juzi.

Dk. Magufuli alifariki Machi 17, mwaka huu, Dar es Salaam. Kabla ya kuzikwa, maelfu ya wananchi kutoka mikoa mbalimbali na nje ya nchi walishiriki kumuaga katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Zanzibar, Mwanza na hatimaye Chato.

Ukiachilia mbali maelfu ya wananchi waliojitokeza kumuaga, wengine walikuwa wakifuatilia tukio hilo kupitia runinga ambazo zilikuwa zikirusha mubashara.

Kwa jinsi maelfu ya wananchi walivyojitokeza huku wakiwa na majonzi makubwa, ni ishara kwamba walimpenda Dk Magufuli kutokana na alivyojiopambanua kwamba ni mpigania haki za wanyonge.

Marais 10 walioshiriki mazishi ya kitaifa yaliyofanyika jijini Dodoma, walimwelezea Hayati Dk. Magufuli kama shujaa wa Afrika ambaye ameonyesha njia kwamba nchi za Afrika zinaweza kuendesha mambo yao pasipo kutegemea wafadhili ambao wanapokupa msaada wanakuwekea masharti. Lakini wakati dunia ikishikwa na butwaa kutokana na kifo cha Dk. Magufuli, wako baadhi ya watu kwa sababu zao binafsi, wengine za kisiasa, wamekuwa wakikebehi kifo cha kiongozi huyo.

Mfano, mapema wiki hii, nikisikiliza redio moja ya nje iliyokuwa ikimhoji Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe. Katika mazungumzo yake, alisema ni idadi ndogo ya watu wanajitokeza kumuaga Dk. Magufuli.

Pia Zitto alizungumza mambo mengine ambayo kwangu niliyaona hayana afya kwa mustakabali wa nchi yetu. Watu aina ya Zitto wako wachache na wengine wanazungumza hayo wakiwa nje hali wakijua kuwa Tanzania ni nchi ya amani na itaendelea kuwa na amani. Wakati Zitto akisema hayo ilikuwa siku ambayo wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam walikuwa wakimuaga mpendwa wao. Nadhani kauli ya Zitto ni ya kisiasa zaidi ambayo kimsingi haina uhalisia na pengine kwangu namwona kiongozi huyu wa chama cha siasa amekosa busara na utamaduni wa Kitanzania. Mtu akifariki dunia haitakiwi kusemwa mambo mabaya juu yake.

Zitto ambaye wakati mwingine nimekuwa nikimfurahia kwa jinsi anavyotoa changamoto kwa serikali, kwenye tukio hili la msiba wa Dk. Magufuli naona ni kama aliamua kuziweka akili zake pembeni, hivyo kuzungumza maneno ya ovyo kwenye hiyo redio ya nje.

Nadhani sasa atakuwa amepata somo kwa jinsi alivyoshudia maelfu ya wananchi walivyofurika kumuaga shujaa wetu, Dk. Magufuli ambaye hata marais waliofika kwenye mazishi ya kitaifa walimzungumzia kwa mambo mazuri aliyoyafanya katika nchi ya Tanzania.

Kimsingi, nchi hii ilipokuwa imefikishwa ilikuwa hatari ndiyo maana nadiriki kusema watu hao wakati wanakula rushwa hawakutarajia Magufuli atakuja. Wakati wanasema Afrika hakuna nchi ya kufikia uchumi wa kati katika awamu moja tu hawakumwona Magufuli kama ataliweza hilo.

Waliposema ujenzi miundombinu katika nchi za Afrika hauwezi kukamilika kwa wakati na kwa bajeti ya ndani, hawakumwona Magufuli na waliposema njia pekee ya kufikia maendeleo yetu ni kufuata masharti magumu ya taasisi za kifedha za kimataifa ambayo yameshindwa kuisaidia Afrika na kuiacha katika giza totoro kwa kuumizwa na madeni makubwa, hawakujua kuwa Magufuli atakuja.

Hayo yalikuwa baadhi ya maneno yaliyotolewa na Rais wa Malawi, Dk. Lazarus Chakwera, wakati akitoa salamu za rambirambi. Pia nilisikiliza hotuba za marais wengine, hakika Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, ni Mwanadiplomasia. Alitoa hotuba ya kiongozi mkubwa kwa hadhara kubwa.Hotuba yake iliakisi hotuba za viongozi wakubwa duniani.

Nilivutiwa pia na hotuba ya Rais wa Kenya, Uhuru Kenyata, mwanasiasa nguli na kitendo cha kusimama dakika kadhaa kupisha Adhana iliyosikika kutoka msikiti wa Gadaffi jirani na Uwanja wa Jamuhuri ni tukio kubwa sana lililotukumbusha heshima kwa mungu wetu na dini zetu, ni heshima kwa imani na heshima anastahili Muumba wetu. Asante Rais Kenyata.

Hotuba zingine za marais wa Afrika kama ile ya Rais wa Afrika Kusini na Rais wa Namibia zimetukumbusha kuwa Afrika bado inatuhitaji tusiendelee kuwa wanyonge, Afrika inatambua mchango mkubwa wa Tanzania katika ukombozi wa nchi nyingine. Hotuba zao zimetukumbusha Ukubwa wa Tanzania katika Afrika. Kubwa zaidi umuhimu wa Lugha ya Kiswahili kwa Afrika kama Dk. Magufuli alivyopenda kukitumia. Tuliobaki ni wakati wetu kuenzi na kuendelea pale alipoishia Hayati Rais Magufuli kusukuma lugha yetu ya Kiswahili Afrika.

Naweza kusema Magufuli katuachia Watanzania hasa vijana fursa ya kwenda kote Afrika kufundisha na kukuza uchumi wetu na wa taifa letu kupitia Lugha ya Kiswahili.

Kwa maoni na ushauri tuwasiliane katika barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AFRIKA**

## DARASA LA NDOA

# Namna ya kutawala msongo wa mawazo - 3



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

KATIKA sehemu ya kwanza na ya pili ya makala hii, tulijadili maana ya msongo wa mawazo, visababishi vyake na athari zitokanazo na msongo wa mawazo kwa mwanadamu.

Pia tulijadili njia za kukabiliana na kutawala msongo wa mawazo zikiwamo kumshirikisha Mungu, kufanya mambo kwa juhudi na maarifa, kuwa na malengo katika maisha, kula chakula bora na kutoa madukuduku yaliyo moyoni badala ya kukaa nayo.

Njia zingine ni kuwatembelea marafiki na ndugu wanaokufanya upate furaha, kuwa na mazoea ya kucheka, kufanya mazoezi, kufanya matembezi na kutafuta chanzo au sababu zinazofanya uwe na msongo wa mawazo.

Katika mwendelezo wa makala hii ambayo ni sehemu ya mwisho, tunadadavua zaidi njia zingine za kutawala msongo wa mawazo ambazo ni; -

**Kuchunguza uhusiano**

Katika maisha, angalia uhusiano wako na watu wengine ukoje mfano mumeo, mkeo, watoto, walezi au wazazi, majirani, mchumba, ndugu, marafiki, na wafanyakazi wenzako. Jitahidi kuwa na uhusiano mwema na watu wengine, itakusaidia. Pia Usiwe mtu wa shari na visasi.

**Mtazamo au fikra chanya**

Uwe na mtazamo au fikra chanya kuhusu maisha yako na watu wengine. Jitahidi kuushinda ubaya kwa wema. Epuka kujikinai, kujikataa na kujiona kuwa wewe ni dhaifu au bora sana kuliko watu wengine.

**Samehe na kusahau**

Usishinde na kulala na hasira hadi kesho. Omba msamaha, samehe na kuachilia. Msamaha huondoa dukuduku. Pia huleta afya ya mwili na roho kwa mkosaji na mkosewa. Msamaha ni lango la baraka na uwepo wa Mungu katika maisha ya mtu.

**Lia**

Ukipatwa na machungu nafsini na ukijisikia hali ya kulia, Lia tu! Kisaikolojia, kulia ni tiba inayopunguza sana uchungu nafsini.

**Pumzika**

Kumbuka kuwa muda wa kupumzika hautatokea usipoutengeneza, hivyo, kupumzika ni agenda ya Maandiko Matakatifu ya Mungu. Kama Mungu mwenyewe aliona umuhimu wa kupumzika, sisi ni nani tusiotaka kupumzika?

Je, kwa kutotaka kupumzika kwetu tutazimaliza kazi zetu au majukumu yetu? Kutopumzika ni kumkosea Mungu na Neno lake. Aidha, ni kujikosea wenyewe! Tufanye kazi kwa bidii na maarifa lakini tusisahau kupata muda wa kupumzika. Kupumzika kunaimarisha na kuboresha afya ya mwili, akili, roho na utendaji wetu.

Asiyependa kupumzika, anapunguza ufanisi wa utendajikazi wake; uwezo wa kufikiri vizuri; anachosha mwili na kudhoofisha afya yake; anajifilisi na kujimaliza pole pole, hivyo, kupunguza siku za kuishi duniani. Haitatokea siku kazi zikaisha. Sana sana kazi zinaongezeka siku kwa siku.

Tutafanikiwa kupunguza kazi lakini si kuzimaliza. Pale mtu atakapoitwa na Mungu kutoka katika maisha haya, ndiyo utakuwa mwisho wa kazi kwake.

**Chukua likizo**

Jipe likizo hata kama umejiajiri. Kama ni mwajiriwa, ukifika wakati wa likizo, nenda likizo. Na ukichukua likizo, pumzika. Baadhi ya watu kuchukua likizo ni kubadili aina ya shughuli au kazi. Matokeo yake, unakuta mtu anarudi kazini akiwa mchovu zaidi kuliko ilivyokuwa kabla hajaenda likizo.

Mwili si chuma. Mwili una mfumo wake. Mwili ukikujulisha kuwa umechoka na unataka kupumzika, usilazimishe! Utii! usije ukapumzishwa kwa lazima katika hali ngumu. Mwili ukichoka, akili na nafsi huchoka pia. Mwili unahitaji muda wa kupumzika. Kumbuka kupumzika kunatupa nguvu na uwezo mpya wa kutenda.

**Mpangilio mzuri wa familia**

Kwa wale walio katika ndoa ni muhimu kumwomba Mungu awajalie watoto watakaomudu kuwatunza na kuwalea vizuri na ambao watapishana vizuri. Si busara kutamani kuwa na idadi kubwa ya watoto ambao hutamudu kuwatunza na kuwapatia mahitaji yao ya msingi ya maisha.

**Pangilia kazi zako vizuri**

Watu wengine wanapata msongo wa mawazo kwa sababu ya mpangilio mbaya wa kazi zao. Panga kazi zako vizuri kwa kuzingatia vipaumbele (priorities). Usifanye mambo mengi kwa wakati mmoja. Unajichosha na utakufa haraka. Kama ni mwajiri, pangilia majukumu ya wafanyakazi wako vizuri ili usiwasababishe msongo wa mawazo utakaoathiri utendaji wao na maisha yao.

**Jiandae mapema kustaafu**

Wafanyakazi wengi katika nchi za kiafrika wana uwezekano wa kufa muda mfupi baada ya kustaafu kwa sababu ya kutofanya maandalizi ya kustaafu.Vijana wa leo watambue kuwa, siku mtu anapoanza kazi, ndiyo siku ya kuanza kufanya maandalizi ya kustaafu. Kustaafu kunaanzia pale unapoanza kazi iwe ya kuajiriwa au kujiajiri. Kumbuka, mfanyakazi wa sasa ni mstaafu na mzee mtarajiwa.

Kufanya kosa la kutojiandaa kwa ajili ya kustaafu ni kosa baya. Ikumbukwe kuwa, leo ya mipango ni kesho bora. Waingereza wanasema, "Planning today, avoids crisis tomorrow." Kujiandaa kabla ya kustaafu ndiko kunako kutengenezea maisha bora baada ya kustaafu na kukuepusha na matatizo yasiyo ya lazima.

Dk.Mkumbo Mitula katika kitabu chake kiitwacho,"Ninastaafu Kazi, Sistaafu Maisha," anasisitiza akisema, "Uzee unakuwa zawadi ukijiandaa; Uzee unakuwa mkosi usipojiandaa."

Wengine wakistaafu wanajishughulisha na shughuli nyingi sana kuliko hata walipokuwa kazini. Hii si sawa kiafya. Jishughulishe kistaafu na si zaidi ya ustaafu. Ifike mahali pa mtu kukubali kuwa sasa uwezo na nguvu vimepungua, hivyo ni muhimu kufanya kazi nyepesi zisizochosha sana mwili na akili.

**Hitimisho**

Msongo wa mawazo ni hali halisi ya maisha ya binadamu ambayo hutokana na mchanganyiko wa hisia. Athari za msongo wa mawazo ni kubwa. Hivyo ni muhimu kujua namna ya kukabiliana na msongo wa mawazo kwa ustawi wa familia na maisha yako. Kumbuka, huwezi kuwa tofauti na uamuzi uliyofanya.

**• Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.**

# MAISHA

Machi 28, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




MAGAUNI YA HARUSI YALIYOSHONWA KWA KITENGE YANAVYOONEKANA KATIKA PICHA TOFAUTI

## HARUSI

Ukurasa 12

## Fahamu faida ya samaki

Ukurasa 14





Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

NG`ARISHA USO WA MBELE WA NYUMBA



## MATITI MAKUBWA

# Mwonekano unaopendwa na watu wengi

Ukurasa 14

# Usijilaumu, usimlaumu mtoto jirekebisheni

Na Moses Ismail

Ni hali inayojitokeza kwa wazazi na watoto wengi, na kila inapotokea mzazi na mtoto kila mmoja kwa wakati wake hutafuta sababu ni nini kimewafanya wawe katika hali hiyo.

Kwa vijijini, wazazi wengi hutafuta sababu za chanzo cha kutoelewana na watoto wao kupitia kwa waganga wa kienyeji. Wanachoamini wao ni lazima kutakuwa na mkono wa mtu. Iweje wao na watoto wao wasielewane?

Wanafanya hivyo pale wanapoona watoto wao wakubwa, wenye uwezo wa mali na fedha, wanashindwa kuwasaidia hata kwa mambo yao madogo tu yanayohitaji fedha. Wanaamini hilo haliwezi kutokea bila ya 'mkono wa mtu'.

Hilo limewahi kutokea baina ya Edith Mgaya, mkazi wa Chamazi, nje ya jijini Dar es Salaam. Yeye na mwanae hawakuwa wakielewana kabisa.

Edith anasema: "Ilifikia mahali mwanangu alikuwa hakanyagi nyumbani hata miezi minne mpaka mitano, namuona tu anapita barabarani na gari yake."

Edith akahisi si bure, lazima kuna mkono wa mtu kwa sababu mtoto wake alikuwa na uwezo mkubwa wa mali, akaenda kwa mganga. Anasimulia:

"Kumbe alikuwa amelogwa. Mganga akanipa dawa. Akaniambia nimuite na nijaribu kuongea na mwanangu kwa upole



wakati natumia dawa hiyo. Leo ni mwaka wa sita sasa hatujakwaruzana."

Ni kweli, kwa imani za kiroho uchawi upo na hata vitabu vitakatifu vinaeleza madhara yake na vinakataza waumini kushiriki uchawi, lakini je, katika hili la mzazi na mtoto 'kuwa mbalimbali' ni uchawi ndio unaosababisha?

"Jibu haliwezi kuwa la moja kwa moja", anasema Denis Munga, mtaalamu wa masuala ya saikolojia na kufanua:

"Haliwezi kuwa la moja kwa moja kwa sababu pamoja na kwamba uchawi upo na watu wanauamini, lakini katika kesi nyingi za mzazi na mtoto kutoelewana suala la saikolojia linachukua nafasi kubwa sana".

Munga anatoa mfano: " wazazi wenye tabia ya kupenda kutokaa pamoja na watoto wao, hawa wanajenga tatizo hilo wenyewe. kutopenda kuwa karibu na mtoto wako wakati akiwa mdogo kunajenga ufa baina yenu.

"Ufa huu ukiendelea kwa muda mrefu, yanakuwa ni maisha ya kawaida baina ya mzazi na mtoto, hata kama mtoto atakuwa na umri wa miaka hamsini, kwa sababu msingi ulishajengwa tangu utotoni".

Wazazi wengi wanaoshindwa kushirikiana na watoto wao katika hali ya utu uzima wanavuna matunda ya ukali waliuonyesha kwa watoto wao walipokuwa wadogo.

Hii inasaidia kwa wazazi wa kizazi hiki kujifunza jambo hilo na kurekebisha pale wazazi wao walipojikwaa kwa malezi yao.

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

## QUIZ

### Le quiz du week

1. Weka maneno yafuatayo katika mtitiriko utakaoyafanya yalete maana kamili.
Mfano: marguerite/est/La/fleur/une →La marguerite estune fleur.

a) oiseau/Le/un/est/perroquet
........................................

b) plantesfragiles/Les/rosiers/des/sont
........................................

c) un/saumon/poisson//est/Le
........................................

d) est/erable/arbre/un/L'
........................................

e) citron/est/Le/fruit/un
........................................

f) poireau/un/est/Le/legume
........................................

g) des/Le chien et le chat/animauxdomestiques/sont
........................................

h) bambou/une/Le/est/herbe
........................................

i) qui/méne au success/est/Le/un/pont/fragile
........................................

j) c'est/l'histoire/qui commence/Entre/au depart/nous
........................................

k) d'avoir/Sois/raison/et puis/sûr/vas-y
........................................

l) la durée/le soleil/de la nuit/apparaîtra/Quelquesoit
........................................

2. Jibu kama kwenye huo mfano hapo chini. Mfano: Tu as une valise? – Oui, j'aiune valise de mon frère.

- Vousavez des chaussures de marche? – Oui, j'ai.......chaussures de monpère.
- Tu as un appareil photo? – Oui, j'ai..........appareil photo de moncopain.
- Vousavezunetente de camping? – Oui, j'ai............tente de mon cousin.
- Tu as unevoiture? Oui, j'ai........voiture de mes parents.
- Tu as des skis? – Oui, j'ai.......skis de ma sœur.
- Vousavezun sac à dos? Oui, j'ai........sac à dos de ma tante.
- Tu as unstylo? Oui, j'ai........stylo de monvoisin.
- Vousavezuneboisson à consommer? Oui, j'ai.......boisson de ma petite amie.
- Tu as des lunettes? Oui, j'ai........lunettes de monami.


Les articles partitifs
Angalia kwa makini mfano huu wa "articles partitifs" katika maelezo yafuatayo, kisha ujibu maswali yatakayofuata kuhusu hizo "articles partitifs".
N.B. (ms) nimasculinsingulier, (fs) nifémininsingulier.
.Cestgentil à toi de faire les courses: alors, s'ilteplaît, tuachetesdu riz (ms), del'eau (fs), de laviande (fs) et de l'huile (fs) et tuprendsde l'argent (ms) dansmon sac.

1. Malizia maneno yafuatayo kwakutumia "articles partitifs" zinazoendana.
→ Du poivre (ms)
→ ........jambon (ms)
→ ........huile (fs)
→ ........parfum (ms)
→ ..........fromage (ms)
→ ..........crème fraîche (fs)
→ ..........pâté (ms)
→ .........bière (fs)
→ ..........vinaigre (ms)
..........rouge (ms) à lèvre
→ ............saucisse (fs)
→ .............sucre (ms)
→ ............eau de toilette (fs)
→ ............beurre (ms)

2. Chaguajibusahihikatikamabanokukamilishasentensizifuatazo.
Le matin, je prends (du – de l') café (ms) ou (du – de l') thé (ms) et les enfantsprennent (de la - du) lait (ms) chaud. À midi, à la cantine, je choisissouvent (de la – de l') salade (fs) ou (de la – de l') omelette (fs). Le soir, je prépare (de la – du) soupe (fs), surtoutl'hiver. Nous mangeonssouvent (du – de la) viande (fs) froideou (du – de l') poisson (ms).

## WATOTO


## PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO

**JAMAA wawili walifika Stesheni, wakakuta treni inaanza kuondoka. Wakaanza kuikimbiza, mmoja alifanikiwa kupanda akaondoka**

**Jamaa aliyebaki akaanza kucheka sana mpaka machozi yakamtoka. Watu wakamuullza, unacheka nini sasa wakati umeachwa? Akawajibu: "kinachonichekesha, yule aliyepanda alikuwa ananisindikiza".**



**SWALI**
**Mamba yupo katika kundi gani la wanyama?**

# MAISHA NDIVYO YALIVYO
## Na Flora Wingia



# Hatua za maisha zaweza kufungwa pasipo kujua

KARIBU msomaji katika safu yetu hii. Maisha ni mchakato. Lakini unaweza kujikuta hayaendi na hujui ni kwa nini. Kumbe ipo siri iliyosababisha mkwamo huo. Leo hebu niongelee kidogo mipaka na hatua za kiroho zilizofungwa. Watu wengi mipaka na hatua zao zimefungwa lakini hawaelewi.

Maneno hatua na mipaka yanaambatana kwa pamoja. Hatua ni nini? Hatua ni kile kitendo cha kusogea kutoka eneo moja kwenda lingine.

Na kufungwa hatua zako ina maana unashindwa kusogea au kwenda sehemu nyingine. Hapo mtu anaonekana 'domant'; hawezi kufanya chochote, hawezi kwenda popote.

Wakati huwa hausubiri na kila jambo lina majira yake. Shetani ana uwezo wa kufunga hatua za mtu ili majira ya lile jambo yapite. Maana yake unashindwa kufika pale ulipokusudia.

Nini maana ya mipaka. Ni kizuizi ambacho kinalinda milki yako isiweze kusogezwa au kupunguzwa. Mungu alipowachukua wana wa Israeli kuwapeleka nchi ya Kaanani alimwambia Musa; nimekupa itawale mipaka yake ndiyo milki yako, isipungue wala isiongezwe, kwa maana hapa ndipo umepewa kukaa.

Hatua na mipaka ni vitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Maisha ya mtu kabla hayajaanza yalikuwepo. Hii ni kwa mujibu wa maandiko ya Mungu.

Maisha yako yalishatengenezwa tayari hata kabla hujaletwa duniani. Yeremia 1:5, neno la Mungu linasema, "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa kimataifa". Pia kwenye Isaya 46:10 imeandikwa, "Niutangazaye mwisho tangu sasa, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado;" Kila kiumbe duniani Mungu alishatangaza mwisho wake. Kuna ulimwengu wa roho (usioonekana) na ulimwengu huu tunaouona kwa macho. Ule wa roho ndio ulimwengu mama, ndio unaochipusha mambo yanayodhihirika ulimwengu wa macho ya mwili.

Mungu anataka kila mtu afanikiwe. Ukipata elimu ufanikiwe pia kupata kazi. Ukioa au kuolewa upate pia watoto, nyumba, magari kusiwapo na mipaka yoyote.

Pamoja na ukweli huo, wapo baadhi ya watu ambao kwa sababu zao wenyewe wamekatisha hatma za wengine katika mafanikio yao. Badala ya kufika chuo kikuu, wanajikuta wanaishia darasa la saba au sekondari. Kumbe wapo maadui waliofunga hatua zao mapema ili wasivuke kufika walikokusudia.

Yawezekana ni maagano kwenye ukoo wao kwamba wasome lakini wasivuke kiwango fulani. Au ni maneno yaliyotamkwa kwa chuki kukwamisha maendeleo yao. Maneno yaweza kuwa yalitokana na mzozo kati ya ndugu au wazazi au majirani.

Maneno ni roho, ni nguvu yakitamkwa pasipo kuyafuta husimama na kutimiza kile kilichotamkwa. Hata Mungu wakati wa uumbaji alitamka na ikatokea kama alivyonena.

Mtu anaweza kuzuia hatua zako za mafanikio kwa chuki binafsi. Unastahili kabisa kupandishwa cheo lakini unaachwa eti utamzidi bosi ambaye kiwango chake cha elimu ni cha chini. Hatma yako inapindishwa kwa makusudi.

Watu wengi wamepindishwa hatma zao pasipo wao kujua. Wanaona pale walipo ni sahihi kumbe walishahamishwa kwenye kusudi na hatua zao za mafanikio zimefungwa. Wanabaki pale pale wakati Baraka zao zimezuiliwa au zimehamishiwa kwa wengine.

Watu wengi leo wanafanya kazi ambazo siyo zao. Kwa mfano, tangu ukiwa shule ulipanga kuwa daktari, lakini ajabu baada ya kuingia chuo kikuu ukaacha masomo ya sayansi ukasomea biashara au sheria.

Pale ulipokusudia kufika haikutokea. Wengi leo walipaswa kuwa watumishi wa Mungu badala yake wamekuwa walimu wa sekondari au wanasiasa. Kumbe hatua zimefungwa kufikia malengo yako.

Huwezi kufanikiwa kama unafanya kitu kinyume na kusudi la Mungu. Ndiyo maana unatumia nguvu kubwa kufanya mambo na matokeo yako ni kidogo sana. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mpenzi msomaji wangu, ni muhimu sana kutafakari wapi unaelekea katika maisha yako hapa duniani. Muombe Mungu akusimamishe katika kusudi lake na afungue hatua zako za mafanikio. Hata maadui wakizifunga, yeye ana uwezo wa kutangua makusudi yao. Zaburi 33: 10. "BWANA huyabatilisha mashauri ya mataifa, Huyatangua makusudi ya watu".

Naishia hapa, kwa neema tukutane wiki ijayo. Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Nitumie ujumbe kupitia 0715268581.

**Msomaji wangu, Lazima watu watafute sana nguvu ya Mungu kufuta hayo maneno. Mungu ni mwaminifu, huchunguza mioyo, tukiomba kwa dhati laana za aina hiyo hufutika.**

**Tuishie hapa hadi wiki ijayo. Ukiwa na kisa, maoni, ushauri nitumie ujumbe kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAPP.**

# NAWAZA KWA SAUTI
## Na Salome Kitomari



# Kuwapo udhibiti mikusanyiko mikubwa kuepuka madhara

JUMAPILI iliyopita wakati wa kuaga mwili wa Hayati Rais Dk. John Magufuli katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, watu kadhaa walifariki dunia huku wakiwamo sita wa familia moja kutokana na mkanyagano.

Mkanyagano huo ulijitokeza wakati kila mmoja akitaka kupata nafasi ya kuaga mwili wa kiongozi huyo, lakini hadi sasa hakuna taarifa rasmi ya mamlaka za polisi, wilaya na Hospitali ya Temeke waliotoa taarifa za idadi ya waliojeruhiwa na kufariki dunia.

Taarifa nyingi ni zile zilizoripotiwa kwenye mitandao ya kijamii kwa wanandugu kusambaza picha za wapendwa wao na kueleza walipoteza maisha siku hiyo katika uwanja huo.

Kwenye mitandao ya kijamii, idadi inayotajwa ni kubwa huku Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ikieleza kupokea majeruhi na maiti saba ambao chanzo chake ni uwanjani hapo.

Kwa upande wa Hospitali ya Rufani ya Temeke, hadi sasa hakuna taarifa yoyote rasmi ya majeruhi au maiti, jambo ambalo limezua utata kuwa katika tukio hilo wangapi walifariki dunia na kujeruhiwa.

Tukio hili linaacha funzo kubwa sana kwa Watanzania na mamlaka mbalimbali kwamba kama wazazi wasingepeleka watoto wao uwanjani huenda wasingejeruhiwa au kukumbwa na mauti na au mamlaka zingeweka utaratibu mzuri, wananchi wangeaga na yasingetokea maafa yoyote.

Hakuna ubishi wazazi waliopeleka watoto wao uwanjani ni katika kuonyesha mapenzi mema kwao, kwamba walitamani kuona mwili wa kiongozi wao na kumuaga, ikiwa ni pamoja na kujifunza, ingawa wangejifunza zaidi kupitia luninga na mitandao ya kijamii ambayo inaonyesha matukio yote muhimu kwa urahisi zaidi.

Lakini bado tunatafakari kwamba ilikuwa lazima kuwapeleka watoto kuona maiti? Je, katika mla na desturi zetu, zetu tunapopatwa na msiba watoto hupelekwa au huonyeshwa? Mara nyingi huwa hairuhusiwi isipokuwa watoto wa kuzaa pekee.

Hoja inayojengwa ni kuwa huenda picha ya maiti itawasumbua watoto na wataota mara kwa mara na kuwafanya wasitulie kila wanapokumbuka tukio hilo, lakini wapo wanaoona ni sawa na hakuna shida yoyote wanayopata.

Tukio hili liwe funzo kubwa kwa Watanzania hasa katika mikusanyiko ya kitaifa ambayo siyo lazima kwenda na watoto ambao hawana nguvu za kujitetea na kujiokoa kwenye vurugu zozote.

Mathalani, inapotokea timu za Simba na Yanga zinacheza, baadhi ya wazazi kwa mapenzi mema kwa watoto wao huambatana nao uwanjani na wakati mwingine vurugu hutokea na kuwa na madhara makubwa kwa watoto.

Ni vyema tukio hili likawa fundisho kubwa kwa wazazi na walezi kwamba kwenye maeneo yenye watu wengi siyo lazima kuambatana na watoto, lakini itapedeza zaidi polisi wakiweka utaratibu wa kuzuia watoto kuwapo.

Mkusanyiko mwingine ambao ni rahisi kukuta watu wazima na watoto ni kwenye maonyesho mbalimbali, ambayo ni muhimu watoto kujifunza lakini muhimu mzazi kuwapeleka siku ambazo siyo za kilele cha maonyesho husika ambazo zinakuwa na watu wengi.

Katika kipindi hiki cha ukuaji wa tekonolojia ni muhimu wazazi wakaitumia vyema kwamba watoto waangalie kupitia luninga na utube, kwa kuwa katika ulimwengu huu wa sasa unaona kila kitu kinachoendelea kwa kuwa kinarushwa moja kwa moja.

Lakini funzo kwa mamlaka zenye wajibu wa kulinda usalama wa mali na raia, kwamba lazima kuwe na utaratibu maalum ambao hauna madhara kwa waombolezaji au wachezaji.

Wapumzike kwa amani walioopoteza maisha katika tukio hilo.

Mungu ibariki Tanzani
Mungu Ibariki Afrika

**Tutafakari!**

# MAGAUNI YA HARUSI YALIYOSHONWA KWA KITENGE YANAVYOONEKANA KATIKA PICHA TOFAUTI



Tunachapicha picha za harusi bure wasiliana kwa namba 0717336368, au barua pepe: Moshilusonzo@ Gmail.com" Moshilusonzo@Gmail. com.

# MITINDO





# KUWA HURU NA FURAHA


## VUKA KWA MAVAZI HAYA YANAFAA

JE kama mwanamke wa nguvu, unajiandaa vyema kuhakikisha unapofika siku zako za hedhi unakuwa huru na mwenye furaha?
Kila mwanamke ni lazima kukabiliana na hali hiyo ambayo kimsingi ni muhimu kwake katika kujenga afya.
Hata hivyo, wengi imekuwa vigumu kujua kitu gani cha kufanya ili awe na furaha zaidi katika kipindi hicho, ambacho kinakuwa na wasiwasi mwingi na kumnyima uhuru mtu kufanya shughuli zake kama kawaida.
Unachotakiwa kufahamu kwanza ni lazima kujua mzuguko wako ili uweze kujiandaa kwa mambo mbili mbali.
Wanawake wengi wanapata hali hiyo kati ya siku 28 ya mzunguko, na hudumu kwa muda wa siku tatu hadi saba.

UNAJIANDAAJE KIMAVAZI?
Kama mwanamke wa kiafrika ni muhimu kutembea na taulo zako ndani ya mkoba katika siku hizo ili kuwa tayari na chochote.
Usisahahu kutembea na mtandio pindi utokapo toka nyumbani ili chochote kitakachokutokea uwe tayari kujisitiri bila wasi wasi wowote.
Hakikisha katika kipindi chote unavaa nguo za rangi nzito ambazo zinaweza kukuweka imara zaidi.
Rangi inayopendekezwa ni bluu, zambarau, nyeusi na kijani.
Pia nguo aina ya jeans zenye rangi za giza zinafaa zaidi kutumiwa katika kipindi hicho.
Unapovaa nguo za aina hii, hautapata shida wala hofu pale unapotembea au kuwa katika mikusanyiko ya watu.
Unaweza kuvaa sketi ndefu yenye kitambaa kizito na rangi za giza, lakini hakikisha sodo yako umevaliwa sahihi na kushikiliwa vizuri na nguo ya ndani.
Sweta la aina hii, inaweza kuvaa na jeans, suruali ya kitambaa au ukatumia kama nguo ya ndani ya suti.

## UREMBO: MATITI MAKUBWA

# Mwonekano unaopendwa na watu wengi



MATITI ya mwanamke licha ya kuwa ni chanzo kizuri cha chakula bora kwa watoto, pia ni moja ya pambo zuri na lenye mvuto.

Kutokana na umhimu wake, matiti lazima yatunzwe ipasavyo kwa ajili ya kulinda urembo wa mwanamke kwa muda mrefu.

Kimsingi kiungo hiki kitaalam ndicho kinampa nguvu mwanamke kutokana na kutunza vitamin nyingi na mafuta ya kutosha.

Wataalam wa masuala ya urembo wanasema kwamba wanawake wenye matiti makubwa, wana mvuto zaidi endapo ataweza kuyatunza vyema.

Wanasema matiti makubwa ni rahisi kumvutia mtu kutokana na mwonekano wake.

Hata hivyo, kuna tatizo kwa wale wenye matiti makubwa kushindwa kuyatunza vizuri na kusababisha kupoteza uzuri wake.

Ifuatavyo ni njia tofauti za kutunza matiti yako na kubaki katika mwenekano ule ule.

**Sidiria ya kutosha**

Wakati wa kununua sidiria, hakikisha unachukua yenye kukutosha vizuri na haina vitu vinavyoweza kukupa michubuko. Hakikisha matiti yako yanakuwa katika hali ya kusimama ili kukupa mwonekano wa kupendeza.

**Weka umbo la kikombe**

Wakati unapovaa sidiria, ni vyema matiti yako ukayaweka katika umbo la kikombe au herufi D, ili kuyafanya yawe kwenye mtanuko wa kupendeza. Aina hii ya utunzaji inapelekea matiti kuonekana na umbo dogo kiasi na unene kiasi.

**Epuka kusafisha kwa maji ya moto**

Kuwa na tabia ya kusafisha matiti baada ya kuoga, hapa usitumie maji ya moto kwa sababu maji ya kawaida huboresha mzunguko wa damu.

Hakikisha hakuna uchafu uliobaki chini ya matiti kwa ajili ya kuepuka harufu mbaya inayotokana na uchafu kuganda.

**Fanya mazoezi ya kutosha**

Hakikisha unafanya mazoezi kila siku kwa ajili ya kuimarisha nguvu ya misuli kwenye matiti. Pia kuogelea ni moja ya zoezi zuri katika kuongeza nguvu na msimamo imara ya matiti.

## MAPISHI Na Mary Geofrey

# FAHAMU FAIDA YA SAMAKI



KATIKA Safi yetu ya mapishi leo, tunaeleza aina za vyakula na faida zake katika afya ya binadamu.

**SAMAKI**

Chakula hiki ni muhimu kwa watu kutokana na kuwa na virutubisho aina ya Omega 3 ambavyo huulinda moyo dhidi ya maradhi.

Samaki pia wana virutubisho vinavyomuongezea mlaji uwezo wa kukumbuka , pia wana virutubisho vyenye uwezo wa kupambana na kansa mwilini.

Wanachangia kuimarisha kinga mwili na kuondoa mafuta makali.

Kutokana na sifa hizo unashauriwa kula samaki kwa wingi kadiri uwezavyo.

Baadhi ya virutubisho muhimu vinavyopatikana kwenye samaki ni pamoja na vitamini D, vitamin 12, Vitamini B3, vitamini B6, Omega 3 Fatty Acids, Protini na madini mengine mengi.

**KAMBA (PRAWNS)**

Chakula cha samaki jamii ya kamba wanafaida kubwa kutokana na kutoa kinga dhidi ya maradhi ya moyo, shinikizo la damu na kuondoa mfadhaiko wa kiakili.

Pia unashauriwa kula kamba angalau mara moja kwa wiki ili kupata kinga ya mwili zidi ya maradhi ya shinikizo la damu.

# MAISHA NI NYUMBA

## Na Elizabeth Zaya

# NG`ARISHA USO WA MBELE WA NYUMBA KWA UMARIDADI



MABORESHO ya nyumba yanapaswa kufanyika mara kwa mara katika kuimarisha ustawi wake.

Mbali na kufanya maboresho kwa ajili ya kujiimarisha, lakini pia kunachangia kwa kiwango kikubwa iendelee kuwa na mvuto.

Leo nataka tuzungumzie namna ya kuboresha nyumba kwenye uso wake wa mbele.

Msanifu Majengo, Mdoe Kimbe, anasema kuna umuhimu mkubwa wa kutofautisha uso wa mbele wa nyumba na maeneo mengine ya nyumba hiyo.

"Kuna nyumba nyingine zimekosa muonekano mzuri wa mbele na hivyo husababisha kushindwa kutofautisha uso wa mbele na wa nyuma wa nyumba au upande wa kulia na kushoto. na hapa ndipo tunasema kwamba kuna haja kwa Msanifu kutumia maarifa kuandaa ramani ambayo itakidhi mahitaji ya nyumba husika," anasema Kimbe.

"Baadhi ya sehemu za mbele za uso wa nyumba ambazo ni muhimu kuzipendezesha ni nguzo ambayo ni sehemu ya jengo iwe ya duara, mstatili au mraba hii itategemea namna ilivyosanifiwa, lakini cha msingi ni kuhakikisha unatengenezwa kwa ustadi mkubwa."

Pia anasema katika kutengeneza uso wa mbele wa nyumba ni vizuri kutumia malighafi ambayo ni rafiki wa mvuto wa macho, imara na ambayo haina madhara kwa binadamu.

"Hili linawezekana kwa sababu Wasanifu wanafahamu malighafi bora za kutumia katika kutengeneza eneo hili kwa hiyo ni vema kuwatumia ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima,"anasema Kimbe.

Mbali na nguzo, Kimbe anasema madirisha nayo ni eneo muhimu ambalo linapaswa kuwekewa urembo hususani lililoko mbele ya uso wa nyumba.

"Na katika kutengeneza dirisha la mbele la uso wa nyumba, hapa napo kutategemea na vigezo vya sehemu au sababu za kisanifu, Msanifu anatakiwa kutumia utaalam wake kupendekeza aina ya dirisha kulingana na malighafi anayotaka kuweka iwe ni kwa mlalo au unyoofu,"anasema Kimbe.

Eneo lingine la kuboresha kwenye uso wa nyumba ni milango ya nje.

"Milango ya nje bila kujali aina zake, hutumiwa kwa kuzingatia aina ya mtiririko wa kisanifu ili kutokupoteza mnyororo mzima wa mtindo na mpangilio wa jengo ulivyo,"anasema.

Kimbe anashuri kwamba, wakati maboresho au matengenezo yanafanywa kwa ajili ya kupendezesha uso wa mbele wa nyumba, ni vema kutokusahau na uchaguzi wa rangi kwenye ukutwa na dizaini katika valanda lake katika uso huo wa mbele wa nyumba.

# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU YA KUCHAGUA ZULIA KUPENDEZESHA SEBULE YAKO

1: Chagua zulia lenye muundo wa kisasa, tafuta usahihi wa aina ya kapeti kama umebuniwa miaka ya hivi karibuni ili kukupa mwonekano wa kisasa.


2: Angalia ukubwa wa zulia kama inatosha kuficha eneo la wazi mbele ya sofa au viti vyako. Lazima uwe na vipimo sahihi vya eneo unalotaka kuweka zulia.

3:Chagua rangi inayoweza kung'arisha na kuongeza ukubwa wa sebule. Inapaswa kueleweka kuwa mazulia makubwa ya rangi nyeusi yanaonekana kupunguza nafasi ya sebule, hivyo chagua rangi nyepesi.

4; Kama nyumba ina watoto, basi unashauriwa kuweka zulia lenye michoro au mapambo ya wanyama, maua au matunda kwa ajili ya kuwafanya wajione wapo pamoja nao.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
R.I.P J.P.M
JUKWAANI
UKISIKIA MZIKI UMEKOLEA, ALAFU SPIKA ZIMEUNGUA KATIKATI YA SHEREHE NDIO HII...
HUU MZIKI MPYA NASIKIA NI BALAA!!!
SASA NDIO MUDA WANGU WA KUTAMBA... NITAJIACHIA KWA SANA
KAKA NAONA KAMA UNAJARIBU KUINGIZA MKONO KWENYE DOMO LA MAMBA!
LIMETOKA JEMBE...SASA NI ZAMU YA 'SHOKA'
INAMAANA HAKUNA KISIKI KIGUMU MBELE YAKE!
RAMLI INASEMA 'JIANDAE KULALA NA VIATU'
KWA HIYO 'HATUPOI?'
BABA ULINIFANYA NIACHE UDOKOZI... SIKUWA MDOKOZI BALI "DOKOZI"
HILI JICHO NAKUHURUMIA WEWE JAMBAZI UNAYEJIONA SASA NI MUDA WA "KUMWAGA LAZI"
KILA JAMBO LINATOA SOMO, SASA LEGEA UONE!
LEGEA UCHEKWE! HAPA KAZI TU.
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MWENYE MSIBA UTAMJUA USONI...

HABARI KIMATAIFA

# Watu 180 wazingirwa na magaidi kaskazini Msumbiji

**MAPUTO,** MSUMBIJI

ZAIDI ya watu 180 wamekwama ndani ya hoteli moja kwenye mji wa kaskazini mwa Msumbiji, baada ya kuzingirwa na wanamgambo kwa zaidi ya siku tatu.

Shirika la Habari la AP limeripoti kuwa watu kadhaa wamekufa na wengine wametafuta hifadhi kwenye kijiji cha Quitunda kilichoko karibu na eneo la mradi wa gesi.

Wanamgambo wa jihadi walianzisha mashambulizi siku ya Jumatano mchana wiki hii, na kuwalazimisha wakazi wa mji huo kukimbilia msituni.

Kulingana na mashirika ya haki za binadamu na watu walioshuhudia, shambulizi hilo limetokea kwenye eneo la Palma karibu na eneo lenye mradi mkubwa wa gesi asilia kwenye jimbo la Cabo Delgado.

Mashambulizi hayo yalitokea baada ya kampuni kubwa ya mafuta ya Ufaransa, Total kutangaza kwamba kazi itaanza tena. Total ni mwekezaji mkubwa katika mradi wa mafuta kwenye jimbo hilo, huku kukiwa na kampuni sita za kimataifa ikiwamo ExxonMobil.

Serikali ya Msumbiji ilisema miongoni mwa watu waliozingirwa katika Hoteli ya Amarula ni pamoja na wafanyakazi wa kimataifa na vikosi vya usalama na kwamba operesheni za kuwaokoa zinaendelea.

Mfanyakazi mmoja wa kampuni ya LNG, alisema takriban mji wote umeharibiwa na watu wengi wameuawa.

Hata hivyo hakufafanua zaidi kuhusu watu waliouawa wala uraia wao.

Shirika la kimataifa la kutetea haki za binaadamu, Human Rights Watch, limesema washambuliaji wana mafungamano na kundi la Al-Shabaab, lakini halina uhusiano wa moja kwa moja na kundi la jihadi la Somalia lenye jina kama hilo.

Watu kadhaa walioshuhudia waliliambia shirika hilo kwamba waliona miili ikiwa mitaani na raia wakikimbia baada ya wapiganaji wa Al-Shabaab kuwafyatulia risasi watu ndani ya majengo yao.

Tovuti ya Afrika Kusini ya News24 iliripoti kuwa raia mmoja wa Afrika Kusini HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/watu-10-wachinjwa-msumbiji/a-44011135" aliuawa wakati wa shambulizi hilo.

Mfanyakazi mwingine kutoka kampuni inayoendeshwa na Total, aliliambia shirika la habari la Ufaransa, AFP kwamba awali helikopta ziliruka katika hoteli hiyo siku ya Ijumaa kujaribu kutafuta njia ya kuwaokoa watu wapatao 180 waliokwama ndani.

Serikali ya Msumbiji ilithibitisha kutokea kwa shambulizi hilo na ilisema wanajeshi wameanzisha operesheni ya kupambana na wapiganaji kwenye mji huo.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi, Kanali Omar Saranga, alisema vikosi vya ulinzi na usalama vinafanya kazi usiku na mchana kurejesha usalama haraka iwezekanavyo.

Ubalozi wa Marekani mjini Maputo, umelaani vikali shambulizi hilo na umeahidi kushirikiana na serikali ya Msumbiji kupambana na vitendo vya kigaidi.

**AFP**



Askari wa serikali ya Msumbiji wakilinda watu waliokimbia mashambulizi ya waasi wenye siasa kali katika mji wa Palma, jimbo la Cabo Delgabo nchini Msumbuji **(PICHA: AFP)**

# UN yaibana mbavu Korea Kaskazini

**NEW YORK,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kauli moja limepitisha azimio la kuongeza mamlaka ya wataalamu wa umoja huo wanaofatilia vikwazo dhidi ya Korea Kaskazini. Uamuzi huo umefikiwa saa chache baada ya wajumbe kukutana kujadili hatua ya Korea Kaskazini kurusha makombora mapya yaliyopigwa marufuku.

Siku ya Alhamisi, Korea Kaskazini ilirusha baharini makombora mawili kutoka pwani yake ya Mashariki, kwa mara ya kwanza tangu Rais wa Marekani, Joe Biden alipoingia madarakani Januari 20. Azimio hilo limepitishwa baada ya kamati ya vikwazo ya Umoja wa Mataifa inayoifuatilia nchi hiyo yenye silaha za nyuklia kuwataka wataalamu kuchunguza urushaji wa makombora uliofanywa na nchi hiyo.

Katika hatua nyingine, nchi za Umoja wa Ulaya ambazo ni wanachama katika Baraza la Usalama zimetoa wito wa kujadiliwa hatua hiyo ya Korea Kaskazini.

**DW**

## Jeshi la Ufaransa lashutumiwa kuua raia

**BAMAKO,** MALI

JESHI la Ufaransa limefanya mashambulizi ya anga dhidi ya kundi la wanamgambo kaskazini mashariki mwa Mali.

Hata hivyo, muungano wa waasi nchini Mali, umedai kuwa shambulizi hilo limewaua takriban raia watano, wakiwamo watoto.

Mashambulizi hayo yalifanywa na kikosi cha Ufaransa cha Barkhane shidi ya kundi la kigaidi la Tuareg.

Kundi la waasi linalojulikana kama Muungano wa Vuguvugu la Azawad, lililaani vikali shambulizi hilo la anga na limetaka uchunguzi wa kimataifa ufanyike.

Hii ni mara ya kwanza jeshi la Ufaransa kushutumiwa kwa kufanya shambulizi lililosababisha vifo vya raia.

Watu kadhaa wameandamana kwenye mji mkuu wa Mali, Bamako jana wakitaka kuondoka kwa jeshi la Ufaransa, baada ya shambulizi hilo kuwaua raia.

**DW**

## Kenya yatangaza masharti mapya kudhibiti corona

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya Uhuru Kenyatta, ametangaza kuweka zuio la watu kutotoka nje ya kaunti tano, katika juhudi za kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona.

Tangazo la zuio hilo ikiwamo watu kutotoka na kuingia katika kaunti hizo litahusu pia mji mkuu wa Nairobi, kwa lengo la kupambana na ongezeko la maambukizi ya ugonjwa huo.

Kaunti zingine ambazo zimeathiriwa na tangazo hilo ni Kajiado, Kiambu, Machakos na Nakuru, huku muda wa watu kutotembea utakuwa kuanzia saa 10 alfajiri hadi saa mbili usiku.

Rais Kenyatta alisema lengo la masharti haya mapya ni kudhibiti maambukizi ya Covid 19 ambayo yameonekana kuongezeka.

Aidha, uuzwaji wa pombe katika kaunti hizo umepingwa marufuku.

Masharti haya mapya yalianza kutekelezwa kuazia saa sita usiku wa jana.

## MAKALA

# AHADI ZA MISIBANI



Na Magabilo Masambu

**Huruma hizo huonyeshwa kwa watoto na familia kwa ujumla. Katika hali ambayo si ya kawaida, ndugu, jamaa na marafiki huwa wanatoa ahadi kemkem kwa familia ya marehemu mbele ya umati mkubwa uliofika katika mazishi.**

WAKATI tukiendelea kuomboleza msiba wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati John Magufuli, ni vyema pia kujikumbusha mambo ambayo mara nyingi yamekuwa yakijitokeza siku na wakati wote wa misiba mbalimbali ya ndugu zetu.

Ni ukweli usiopingika kwamba nyakati za misiba huwa zinakuwa ngumu kutokana na uhusiano kati ya wale tunaobaki na wale tunaowaaga. Kipindi hiki cha msiba, kila mtu huwa anaingiwa na huruma hata kama unayemuaga hamkuwa na uhusiano mzuri. Hii hutokana na hali ya ubinadamu tulio nao ndani mwetu.

Bahati mbaya tu tuliyo nayo ni kwamba umekuwa utamaduni wa watu wengi kuonyesha huruma kubwa wakati na siku ya mazishi hasa baba anapofariki dunia kwenye familia. Huruma hizo huonyeshwa kwa watoto na familia kwa ujumla. Katika hali ambayo si ya kawaida, ndugu, jamaa na marafiki huwa wanatoa ahadi kemkem kwa familia ya marehemu mbele ya umati mkubwa uliofika katika mazishi.

Wengine huwa wanajitokeza hapo hapo kwamba watawasomesha watoto wa marehemu kama bado wako masomoni, wako wengine huwa wanajitokeza na kusema kwamba watawachukuwa na kuwasaidia kiwango kile kile ambacho baba yao angeweza kuwasaidia na kadhalika.

Basi kupitia ahadi hizo, wajane na watoto wao hufarijika sana kwa kusikia hivyo na kwamba faraja ile ile waliyokuwa wanaipata akiwapo marehemu baba yao itakuwapo. Msiba ukiisha watu huaga na kurejea kwao.

Nimewahi kujiuliza, hivi kwa upendo ambao mara nyingi watu huonyesha kwenye misiba, watakavyoijali familia ya marehemu kesi nyingi za mirathi zilizoko mahakamani na zile za malalamiko ya ndugu kudhulumu mali za familia hizo huwa zinasababishwa na kina nani? Nikaja kugundua kumbe ni ndugu, jamaa na marafiki wale wale wanaotoa ahadi nyingi za kuwasaidia watoto wa marehemu.

Wako pia ambao maisha yao kwa asilimia zote yaliwezeshwa na marehemu nao huwa wakishaona aliyewawezesha amekwishafariki dunia, huwa wanakaa kimya milele bila kujitokeza kwenye familia ile angalau kutoa mchango wao ikiwa kama shukrani zao kwa familia kutokana na mchango mkubwa wa marehemu katika maisha yao.

Nafikiri si sahihi kutoa ahadi nyingi juu ya kuisaidia familia ya marehemu au watoto wake lakini baada ya msiba ama tunaitelekeza familia hiyo au tunakuwa sehemu ya manyanyaso katika familia yenyewe.

Tumeshuhudia mara nyingi baadhi familia za marehemu ambao walikuwa maarufu na waliosaidia watu wengi kabla ya kukutwa na umauti zikiteseka, wakati kuna ndugu jamaa na marafiki ambao maisha na mafanikio yao yasingekuwa kama yalivyo bila marehemu kuwawezesha.

Ukitafakari sana ni mambo yanayoumiza. Wengine hudiriki kusema baba yao ni kweli alitusaidia lakini hakuisaidia familia yake, wengine ndiyo kwanza hushiriki kufilisi hata kidogo walioachiwa na baba zao. Watoto wanaanza kuhangaika wengine wanaingia mitaani, wengine wanakuwa walevi na wezi mwisho wanaishia magerezani, wakati kuna watu wengi waliosaidiwa na wazazi wao lakini shukrani ya punda inageuka kuwa mateke.

Wakati tukiendelea kuomboleza msiba mzito huu kwa taifa, tukumbuke pia kwamba kuna misiba mingine mingi ya namna hii, ambayo pia ni mizito kulingana na mapenzi waliyo nayo kwa wapendwa wao. Tusiwe sehemu ya mateso katika familia hizo baada ya wapendwa wao kuondoka.

Inawezekana baba alikuwa jambazi, au muuwaji lakini hizo haziwezi kuwa tabia za familia, kwahiyo si haki kuzihukumu familia hizo kwa matendo ya watu wengine maana kila mmoja atabeba msalaba wake.

Wale tulio karibu kwa maana ya ndugu wa karibu kabisa ambao ndiyo huachiwa dhamana ya kuzilea familia hizo, lazima tutende yanayompendeza Mungu wanasema kipimo tutakachowapimia wengine ndicho tutakachopimiwa.

Pili tusione sasa ndiyo fursa pekee ya kutengeneza maisha yetu kutumia mali zinazoachiwa familia. Wajane wanalia na watoto wao kwa maovu wanayotendewa na ndugu walewale wanaoonekana msaada mkubwa siku za mazishi. Kama mali zitakuwepo zitumike kuendeleza maisha yao ya kwetu tutafute kidogokidogo tutafanikiwa tu.

Mwisho, msiba huu mkubwa utumike kutukumbusha mengi kuhusu kujali familia hizi. Mzee John Pombe Magufuli natambua amesaidia wengi, basi shukrani zetu zibaki kama kumbukumbu katika familia yake.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mchakamchaka shuleni ulivyoleta uzalendo



Na Adam Fungamwango

**Shule zote Tanzania zilikuwa na kipindi cha kukimbia mchakamchaka asubuhi. Zingine mara moja kwa wiki. Kuna zingine mara mbili na hata mara tatu. Mara ya tatu mara nyingi inakuwa Ijumaa.**

UZALENDO siku zote hauanzii ukubwani. Huwezi kuwa tayari mkubwa ukawa mzalendo wa nchi yako. Siku zote uzalendo huanzia utotoni.

Nchi nyingi duniani hufanya hivyo. Huwajenga watoto na vijana wao tangu udogo kuwa wazalendo na wenye uchungu na nchi yao. Ni sawa na kumfundisha mtoto kutokuwa na tabia ya uchoyo. Huwezi kumfunza ukubwani. Utaanza utotoni. Atapewa kitumbua na kuambiwa awakatie wenzake. Hapo taratibu atakuwa anaanza kuachana na tabia ya ubinafsi aliyonayo binadamu tangu anazaliwa.

Watanzania kuna sehemu tulikosea. Ndiyo maana hata aliyekuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, alikuwa akipigia kelele sana suala la uzalendo. Alionekana kushangaa Watanzania wengi wa sasa kutokuwa na tabia ya uzalendo. Wengi ni wabinafsi na wanatanguliza maslahi binafsi badala ya taifa.

Leo tutaangalia moja tu ya mambo ambayo yaliifanya Tanzania huko nyuma kuwa na wananchi wenye tabia ya uzalendo. Mojawapo ni kukimbia mchakamchaka shuleni. Kwa sasa ni aghalabu sana kuona, hivyo kwenye shule za sasa, au halipo kabisa.

Shule zote Tanzania zilikuwa na kipindi cha kukimbia mchakamchaka asubuhi. Zingine mara moja kwa wiki. Kuna zingine mara mbili na hata mara tatu. Mara ya tatu mara nyingi inakuwa Ijumaa.

Huu ndio mchakamchaka mkubwa zaidi au tuseme ndiyo wanafunzi wanakimbia umbali mrefu sana kutoka shuleni na kuzunguka huku na huko kabla ya kurejea. Mchakamchaka uliwafundisha wanafunzi uzalendo kuwa wakakamavu, kupendana, kujaliana, umoja, na kujiona kama ndugu, kusaidiana na mengine mengi.

Uliwafanya pia kuwa werevu darasani, kujiamini, ukichochea ukuaji wa uwezo wa akili kwa mwanafunzi, misuli na mapafu. Ulisababisha kugundua baadhi ya vipaji vilivyojificha kwa wanafunzi kama vile kuimba, au kukimbia.

Na hata wanafunzi wenye matatizo ya kiafya waligundulika kwenye mchakamchaka na kuanza kutibiwa mapema kabla ya ugonjwa kuwa sugu.

Kwa wakati huo wanafunzi wengi walipenda sana kipindi cha mchakamchaka kwa sababu kilionekana na kufanana kama kipindi cha michezo hivi, watu wakikimbia na kuimba Sasa twende kwenye nyimbo zenyewe. Mara nyingi nyimbo ziligawanyika sehemu mbili.

Nyimbo za hamasa, uzalendo wa nchi, kusifia viongozi wa Tanzania na hata wa nje lakini wenye mlengo wa siasa za nchi hii, kuwaponda mabeberu wa Afrika Kusini ambao wakati huo nchi nyingi za Kusini mwa Afrika bado hazikuwa huru.

Upande wa pili zilikuwa nyimbo zilizotungwa tu na wanafunzi wenyewe kutokana na muono wao na mazingira yenyewe wanayoishi. Hazikuwa nyimbo rasmi. Nyimbo hizi ziliimbwa wakati wanafunzi wako mbali sana na shule na hata walimu walikuwa hawazijui nyimbo hizo.

Wanafunzi wanaporudi sasa na kukaribia karibu na maeneo ya shule, ndipo wanabadilisha na kuanza kuimba nyimbo rasmi za shule. Tuanze kwanza na nyimbo rasmi za shule ambazo ziliimbwa na kujulikana Tanzania nzima.

"Iddi Amin akifa, mimi siwezi kulia. Nitamtupa Kagera, awe chakula cha mamba."

"Alisema alisema, alisema Nyerere alisema, vijana wangu wote mmelegea. Sasa tuanze mchakamchaka chinja." Ukiacha na nyimbo hizi kuna ule wa "Panda mlima panda, panda, panda usichoke."

"Kaburu matata hiya hiya...vijana mmechoka? Bado. Mbona hamuimbi? Tunaimba." Ukitoka huo unakuja ule wa "Kimbunga cha nini? Chahamia mpakani."

"Banda aa aa Banda, ana wazimu, Kambona kawekwa Ulaya. Na nani? Na Mwingereza."

Wengi wanakumbuka siasa za Mwalimu Nyerere wakati ule za Ujamaa na Kujitegemea, hivyo alihitifiana na aliyekuwa mmoja wa Mawaziri wake, Oscar Kambona aliyetimkia Uingereza, hivyo baadhi ya nyimbo za mchakamchaka 'zilimnanga' kweli.

Kamuzu Banda yeye alikuwa Rais wa Malawi. Huyu mara kwa mara alikuwa akiichokonoa Tanzania, akidai sehemu ya ardhi ya Tanzania na Ziwa Nyasa ni mali ya Malawi. Na yeye aliipatapata kwenye nyimbo za hamasa.

Kama nyimbo zingekuwa zinaua, huyu angekufa kwa nyimbo tu, yeye na Nduli Addi Amin.

"Zaina Zaina mtoto wa Ngaza, unanichanganya, nipe raha Zaina." Hapa sasa zinaanza zile nyimbo za kutungwa na wanafunzi wenyewe.

"Daladala Simba Luwala, chini zenge, juu makaratasi." Hawa ni wanafunzi wa Dar es Salaam, wakiliimba daladala moja maarufu sana enzi hizo,' Simba Luwala.'

"Kanyaga twende, limbwata limbwata. Ng'ombe wangu ana miguu wa bia." Halafu kuna ule wa "Mama mende, mama panya." Huu ulitokana na tangazo moja maarufu redioni miaka ya katikati ya 1980, wanafunzi wakaufanya wa kukimbilia mchakamchaka.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora, Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyota IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini alimteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

LENGO halikuwa baya kama walivyodhani. Ilikuwa baada ya hapo apigiwe simu tu baba mtu aende alipo mtoto ndiyo akutane na mkewe Ester na familia yake ili kuangalia mustakabali wa mke na mtoto.

"Iliposhindikana kumpata bwana huyu, tukawa tunajiuliza sasa tutamrudisha vipi, ndipo nilipokutana na watu ambao waliniunganisha na huyu dada na tulipokuwa tunaongea, tukajikuta wote sisi ndio wenye mkasa huu. Mimi ndiye niliyetelekezwa na mtoto na yeye ndiye mtoto wake alitekwa. Nikamchukua na kwenda kumkabidhi mtoto wake nyumbani kwangu." Ester akazidi kupasua.


"Mimi sina ugomvi na huyu dada, japo Ben aliniacha mimi na kwenda kumuoa huyu kwa ndoa ya kiserikali, ndiyo maana wote wawili tukaungana ili kuikomesha hali hii ya kudhalilisha wanawake. Wanawake tunafanywa kama buyu la asali. Mtu anachovya hapa, halafu akichoka anaacha anakwenda kuchovya kwingine.

"Leo nimekuja hapa kumtetea shoga yangu kuwa wala hana hawara wala nini ni mimi niliyetelekezwa, ndiye niliyesababisha mtoto wenu atekwe na siyo kama nina mpango tena wa kutaka kuendelea kuishi naye. Mimi nina uwezo wa kuendesha maisha yangu bila yeye. Siwezi kurudiana naye. Mtoto wenu Tina yupo nyumbani na ana afya tele."

Kimya kilitawala. Kila mmoja alikuwa akivuta picha jinsi tukio lile lilivyotokea. Kumbe mke wa zamani wa Ben ndiye aliyesababisha hayo. Kisa Ben alimtelekeza. Neema aliingia kwenye mzozo mkubwa kutokana na uamuzi wa Ester. Akaambiwa kahaba. Hawara yake ndiye aliyemteka mtoto.

Ben tayari alikuwa amempa talaka Neema. Kumbe ilitolewa kimakosa. Ester tayari ameshasema kuwa hana tena mpango wa kurudiana na Ben. Neema naye ana talaka mkononi. Ilikuwa pigo kubwa kwa Ben. Tayari alishaanza kuona makosa yake. Papara, hasira na wivu vilimponza.

Angesubiri kidogo asingetoa talaka kwa pupa. Kumtuhumu mkewe Neema kuwa huenda alikuwa na mwanamume nje ambaye alimteka mtoto lilikuwa ni kosa kubwa.




**Pamoja na kuwaomba radhi wanawake wote wawili, pamoja na ndugu zake kwa yote aliyoyafanya, haikusaidia. Haikuwafanya Ester na Neema kumsamehe Ben.**

"Nashukuru sana shoga'angu Ester. Mimi nimekuita hapa kwa lengo moja tu. Uthibitishe kuwa mtoto hakutekwa kwa hawara yangu. Kumbe mtoto ametekwa si kwa sababu yangu, ila kwa sababu ya Ben. Hakuwahi hata siku moja kuniambia kuwa alikuwa na mke, tena alimuoa kwa ndoa." Sasa ilikuwa ni zamu ya Neema kuielezea familia nini kimetokea na mtazamo wake.

Ben hakuona kama anaweza kuokoa chochote pale. Tayari aliona ameshakosa mwana na maji ya moto.Ester na Neema wameungana. Walipoungana yeye hapajui.

"Walionana wapi hawa?" Alijiuliza.

Alimuoa Ester. Akamtelekeza. Ni kutokana na penzi jipya la Neema. Lakini kwa kilichotokea aliona kabisa yuko karibu kukosa kila kitu.

Pamoja na kuwaomba radhi wanawake wote wawili, pamoja na ndugu zake kwa yote aliyoyafanya, haikusaidia. Haikuwafanya Ester na Neema kumsamehe Ben. Na hata Neema ambaye ndiye aliyekuwa anaishi naye kwa sasa.

"Kumbe haya yote yamesababishwa na wewe Ben. Mtoto ametekewa kwa sababu yako. Wala si kwa sababu ya mkeo kama ulivyotuaminisha sisi ndugu zako." Mzee mmoja ambaye ndiye alionekana kusikilizwa zaidi kwenye kikao hicho alisema. Huyo ni mjomba wao.

"Sijui katekwa na hawara wa mkeo, kumbe si kweli katekwa na mkeo Ester. Huyu ulifunga naye ndoa ya kanisani kwa hiyo bado ni mkeo, ila mmetengana tu na mna mtoto mmoja, Tina. Tena kwa sababu ya akili zako mbovu, umemtelekeza kwenda kuoa mke mwingine Neema. Na kwa sababu ulijua huwezi kumuoa kanisani una kikwazo, ukakimbilia kuoa Bomani. Haya aibu imekukuta. Leo wanawake wako wote wawili Mungu kawakutanisha. Kila mmoja anajua dhambi zako ulizofanya. Umetutia aibu sisi ndugu zako wote." Wakati akiongea maneno hayo, Ben alikuwa anatokwa na machozi.

"Nawashukuru sana wanawake ninyi wenye akili na busara. Ingekuwa wengine wangegombana. Ester usingekuja kumtetea Neema hapa kwa sababu yeye ndiye aliyesababisha uachwe na akaolewa yeye. Na Ester ungeweza kumfanya chochote mtoto Neema kwa hasira ya kutelekezwa, lakini ulimlea kama mtoto wako, hadi ulipomrudisha kwa mama yake.

"Lakini nilichofurahi sana kumbe hukuwa na dhamira ya kumteka kwa kumdhuru, ilikuwa kumlazimisha baba yake aje muelewane, ila tu ilishindikana kwa sababu alikuwa amebadilisha namba za simu kwa kusajili laini nyingine.

"Hata Neema ungeweza kumchukia Ester kwa sababu ndiye aliyesababisha kutekwa mtoto wako Diana. Na amesababisha ndoa yako leo iko shakani na una talaka mkononi. Hamkujali yote. Ninyi ni wanawake mashujaa na mfano wa kuigwa. Ingekuwa wanawake wengine ingekuwa nongwa. Kila mmoja angetaka kujifanya mjuaji na ni zaidi na mwenzake. Mimi nadhani tu itoshe kusema kila mmoja afanya anachojisikia kufanya."

"Wakubwa zangu mimi nimemaliza. Alinitekeza, naendelea na maisha yangu. Ndugu yenu ameoa, siwezi kufanya chochote. Na hata kama kwa sasa asingekuwa na mke, siwezi kurudiana naye tena." Alisema Ester akinyanyuka, tayari kwa kuondoka.

"Nisubiri tuondoke wote shoga." Ilikuwa ni sauti ya Neema. Pamoja na kwamba kila mtu anatambua kuwa lengo la mkutano ule ile talaka aliyopewa na mumewe, hawakudhani kama angeondoka mapema kiasi kile, au mara baada ya kikao.

"Mimi pia naondoka. Nina talaka mkononi. Kama alinipa kimakosa au alikuwa na hasira sijui, lakini kwa yote ambayo ameyafanya, sina haja ya kuishi na mwanamume kama huyu. Kama alimtelekeza mwanamke akanioa mimi, atashindwaje huko mbele ya safari asinitelekeze na mimi? Hapa tu tayari alishaniona ni kahaba, nimesababisha mtoto atekwe. Shoga, ngoja nimvalishe Diana twende zetu."

Walitoka nje ya geti. Kwa mbali Neema aliliona gari lilikuwa limepaki. Wala hakujiuliza mara mbili kuwa ndilo lilimleta Ester nyumbani kwake alipompigia simu na kumwelekeza kuwa aje kwenye kikao hicho kwa ajili ya kuumaliza utata. Lilikuwa la Jerry.

**INAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI

# NYOSHI KUMBE HUKUPATA MISUKOSUKO KWA MAGUFULI



MWANAMUZIKI wa Dansi, Nyoshi El Sadaat, amesema tangu aingie madarakani hayati Rais Dk. John Pombe hakusumbuliwa kuhusu uraia wake.

Nyoshi El Sadaat ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema kiongozi huyo aliwafanya wageni wote waishio Tanzania kuwa salama, uhuru na hawajasumbuliwa kwa jambo lolote.

"Naishi hapa kwa kibali lakini tangu ameingia madarakani sijaona mtu anakuja kunisumbua nyumbani kuhusu kibali changu, aliWAWEKEA WAGeni uhuru wa kuishi vizuri na kwa miaka yake yote wageni tumekaa kwa salama, pia ameleta maendeleo ya hapa ndio maana mataifa mengine walitamani kuwa na kiongozi kama yeye" amesema Nyoshi El Sadaat.

# SHOLO

## ETI MTOTO WA MAGUFULI?



MSANII wa muziki wa Singeli, Sholo Mwamba, amesema tangu afanye shoo zake katika kampeni za CCM, jina lake limebadilika na kuitwa mtoto wa Magufuli.

Hata hivyo, Sholo ameongeza kusema Hayati Dk. John Magufuli amemwachia zawadi ya kitambulisho ambacho anaweza kuingia nacho popote kama msanii.

"Baada ya taarifa kutoka nilipokea simu nyingi sana kwamba baba yangu amefariki, kwa sababu ninavyotembea watu wananiita mtoto wa Magufuli ilikuwa ngumu kuamini kama kweli amefariki" amesema Sholo Mwamba.

## TID MAOMBI YAKO TU YANATOSHA



IKIWA leo siku ya tatu tangu kufanyika mazishi ya aliyekuwa Rais Dk. John Pombe Magufuli, mwanamuziki wa BongoFleva TID, ameomba msamaha kwa kushindwa kufika kwenye maziko yake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, TID ameandika kuwa asamehewe kwa kushindwa kwenda kumzika na anamuomba Mungu amuweke peponi

"Hakika Ijumaa ya leo itabaki kuwa kwenye kichwa changu, maneno peke yake hayatoshi, naomba Allah akusamehe madhambi yako, pia huko ulipo nisamehe kwa kushindwa kufika mazikoni Chato" .

## HABARI MICHEZO



# KANTE
## NJE MECHI MBILI UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

N'GOLO Kanté atakosa mechi mbili za kufuzu Kombe la Dunia za Timu ya Taifa ya Ufaransa kutokana na majeraha.

Kiungo huyo wa Chelsea amepata jeraha la misuli kwenye mchezo wa Les Bleus ambao walikwenda sare ya 1-1 na Ukraine Jumatano usiku.

Hatosafiri kurejea Stamford Bridge kutokana na kufanyiwa upasuaji na Ufaransa imethibitisha habari hizo.

"N'Golo Kante hatokuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa katika mechi mbili zijazo moja ni ya Jumapili dhidi ya Kazakhstani na siku tatu baadaye dhidi ya Bosnia-Herzegovina," taarifa ya Timu ya Taifa ya Ufaransa ilisomeka.

"Kiungo wa klabu ya Chelsea amepata majeraha katika paja la kushoto katika mchezo wa Jumatano dhidi ya Ukraine katika dimba la Stade de France na alifanyiwa vipimo siku ya Alhamisi."

Kante anaweza pia kukosa mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya West Brom utakaochezwa Aprili 3, mwaka huu na ule wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya FC Porto siku nne baadaye.



## UNITED YAJITOSA KUMTAKA LLORENTE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeingia kwenye anga za kiungo fundi wa Atletico Madrid, Marcos Llorente, kwa ajili ya kutaka kumsajili wakati wa dirisha la majira ya joto.

Manchester United imepeleka mezani ofa yake kwa Atletico Madrid kwa ajili ya kupata saini ya mchezaji huyo, kwa mujibu wa AS.

Mashetani Wekundu wanatarajiwa kufanya mabadiliko katika safu ya ulinzi na kuongeza nafasi ya kiungo mkabaji katika dirisha kubwa la usajili, huku kocha Ole Gunnar Solkjaer akitaka kuongeza nafasi zaidi katika eneo la kiungo.

United ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, inapanga kukifanyia maboresho makubwa kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Kikosi hicho kinaonekana kuhitaji wachezaji zaidi kwenye safu ya kiungo na ushambuliaji, kutokana na msimu huu wachezaji wake wengi kusumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara.

Llorente ameichezea Atletico Madrid katika mechi 36 msimu huu akifunga magoli 10 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mashindano yote.

# RASHFORD, BUKAYO WAONDOLEWA ENGLAND

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford na winga wa Arsenal, Bukayo Saka wameondolewa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England kuelekea mechi za kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Albania na Poland.

Wote wawili waliukosa mchezo wa Alhamisi wakati England ikiibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya San Marino pale katika dimba la Wembley.

Rashford mwenye umri wa miaka 23, alijiunga na kikoci hicho cha kocha, Gareth Southgate licha ya kuwa na majeruhi ya mguu na amerudi kwenye kikosi cha United baada ya kufanyiwa uchuguzi wa kina.

Saka mwenye umri wa miaka 19, ameumia misuli na hivyo kumfanya kushindwa kukichezea kikosi hicho.

"Marcus Rashford na Bukayo Saka hawatakuwa katika kikosi cha England katika mechi zijazo za kufuzu Kombe la Dunia 2022," ilisema taarifa ya Chama cha Soka cha England (FA).

"Rashford alithibitika kuwa na majeraha katika Uwanja wa St.Georger's Park ambayo yalimfanya kukosa mchezo dhidi ya San Marino, na tumekubaliana aendelee na matibabu katika klabu yake ya Manchester United.

"Saka amebaki na Arsenal kwa ajili ya uchunguzi zaidi, lakini kwa sasa hatakuwapo katika kikosi kitakachokabiliana na Albania na Poland."

England leo Jumapili watacheza na Albania kwenye mchezo wa Kundi I kabla ya kuwavaa Poland katika dimba la Wembley Jumatano.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RAMOS ASHAURIWA KUSTAAFIA MADRID

●●● Hata hivyo beki huyo hajaonyesha nia ya kuhitaji kubakia katika klabu...

**MADRID, HISPANIA**

GWIJI wa Real Madrid, Fernando Hierro, amesema anatarajia kumwona nyota wa kikosi hicho, Sergio Ramos akiongeza mkataba wa kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Hierro amesema anaamini kwamba beki huyo ataongeza mkataba mpya ambao utakuwa ni wa kuitumikia timu hiyo kwa maisha yake yote.

Mkataba wa Ramos ndani ya kikosi cha Real Madrid unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa msimu huu na hadi sasa suala la mkataba wake mpya linaonekana kuwa bado ni gumu.

"Ninapenda kumwona Sergio Ramos akiendelea kuichezea Real Madrid na kustaafia hapo kwani ni mchezaji mzuri na ana uwezo mkubwa," amesema Hierro akinukuliwa na gazeti la Marca.

Kwa mujibu wa ripoti, Ramos mwenyewe hajaonyesha nia ya kuongeza mkataba mpya na anatajwa kutaka kuondoka kwenye klabu hiyo.

Manchester United na PSG ni miongoni mwa klabu zinazotajwa kuwania saini ya nahodha huyo wa Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania.

Kwa sasa nyota huyo yuko katika kikosi cha Hispania na kocha wake, Luis Enrique ameweka wazi maumivu ya enka aliyopata katika mechi ambayo Real Madrid ilipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Celta Vigo si makubwa.

Maumivu hayo ya Ramso ambaye alitoka kufanyiwa operesheni ya mguu hivi karibuni yalianza kuleta hofu ya kuikosa michezo dhidi ya Ugiriki, Georgia na Kosovo.

## KWA UFUPI

### CHELSEA YAMTAKA LUKAKU

CHELSEA watafikiria kuhusu usajili wa straika wao wa zamani, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27, kama hawataweza kumsajili nyota wa Norway, Erling Braut Haaland (20), kipindi hiki cha majira ya joto. **(Telegraph)**

### LUKAKU AGEUKA LULU

MANCHESTER City pia wanafikiria kumsajili Lukaku, ambaye amefunga mabao 59 kwenye mechi 85 alizocheza pale Inter Milan. (Calciomercato, via Manchester Evening News)

### HAALAND SOKONI RASMI

KLABU ya Borussia Dortmund imetaja ada ya kumuuza nyota wake, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 19 kuwa ni pauni milioni 154. (ESPN)

### SANE: SIONDOKI LIVERPOOL

STRAIKA wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 28, amedokeza kwamba anataka kubakia Liverpool hata kama kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kitashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. (Sun)

### LACAZETTE AWINDWA

SEVILLA na Roma zinawania kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Alexandre Lacazette, ambaye ana umri wa miaka 29. (ESPN)

### PSG YAMGANDA NEYMAR

KLABU ya Paris St-Germain ina matumaini fowadi wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, atasaini mkataba mpya, lakini majaliwa ya Kylian Mbappe bado hayajulikani. Fowadi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake unamalizika mwaka 2022. (Marca)

### LINGARD KURUDI UNITED

MANCHESTER United wanatumaini kiungo wao, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, ambaye anacheza kwa mkopo West Ham, atarudi klabuni hapo katika kipindi cha majira ya joto. (Sun)

### LLORENTE ANUKIA EPL

MANCHESTER United imetoa ofa ya pauni milioni 68.5 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Marcos Llorente mwenye umri wa miaka 26. (AS)

### PEREZ AKASIRIKA

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez ameripotiwa kuwa na hasira sana na Manchester United baada ya jaribio lao la kutaka kumsajili mlinzi, Pau Torres mwenye umri wa miaka 24 kukwama. (El Desmarque, via Mirror)

### KLOPP VS WIJNALDUM

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amewataka wamiliki wa klabu hiyo kufikia makubaliano na kiungo, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, kuhusu mkataba mpya. (90min)

### MALEN AKARIBIA ANFIELD

LIVERPOOL inaongoza dhidi ya AC Milan na Juventus kwenye mbio za kumsajili straika wa PSV, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 22. (Gazetta dello Sport, via Mail)

## HABARI MICHEZO

# NTIBAZONKIZA AISOGEZA BURUNDI AFCON 2022

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Yanga, Saido Ntibazonkiza alifunga bao moja na kuisaidia timu yake ya taifa ya Burundi kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Afrika ya Kati na kusubiri hatima ya kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), kwenye mechi ya mwisho.

Ntibazonkiza ambaye kwa muda mrefu ilielezwa ni majeruhi na kukosa mechi kadhaa za Ligi Kuu Tanzania Bara na klabu yake ya Yanga, alipachika bao dakika ya 58 kwenye mechi ya Kundi E, Burundi ikiwa nyumbani mjini Bujumbura.

Mabao ya Afrika ya Kati yalifungwa na Louis Mafouta dakika ya 40 na 52, kabla ya Ntibazonkiza kufunga dakika ya 58 na Christophe Nduwarugira kufunga bao la pili la kusawazisha dakika ya 80.

Ni matokeo ambayo yanaifanya Burundi kufikisha pointi tano, ikishika nafasi ya tatu chini ya Mauritania yenye pointi sita, ikiwa kwenye nafasi ya pili na Morocco ambayo tayari imeshafuzu baada ya kufikisha pointi 11.

Juzi hiyo hiyo, Mauritania ikiwa nyumbani ililazimishwa suluhu dhidi ya Morocco na kuzifanya timu hizo kugawana pointi moja moja, kila mmoja akisalia kwenye nafasi yake ya kwanza na ya pili.

Ntibazonkiza na wenzake watakuwa na kibarua kingine siku ya Jumanne, Machi 30, mwaka huu watakapokuwa nchini Morocco kucheza dhidi ya wenyeji na wakihitaji ushindi ili wafuzu, kwani watafikisha pointi tisa, lakini pia wakiiombea Mauritania ambayo nayo itakuwa ugenini dhidi ya Afrika ya Kati ifungwe.

Afrika ya Kati ambayo inashika mkia ikiwa na pointi nne, nayo ikishinda itafikisha pointi saba, hivyo chochote kinaweza kutokea katika kundi hilo.

Kwa upande wa Tanzania (Taifa Stars), yenyewe imeshapoteza nafasi ya kushiriki fainali hizo baada ya kukubali kufungwa na Equatorial Guinea, hivyo leo itashuka dimbani kuwakaribisha Libya katika mechi ya Kundi J ili kukamilisha ratiba.

Mechi nyingine ya kundi hilo la Taifa Stars itakuwa ni kati ya vinara Tunisia na Equatorial Guinea ambazo tayari zimeshakata tiketi ya kucheza AFCON hapo mwakani.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kujiandaa na mechi za kuwania tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (AWC), zitakazochezwa baadaye mwaka huu. **PICHA: TFF**

# Gwambina yajipanga 'kupasha' viporo

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kuondolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Mohamed Badru amesema wameongeza nguvu katika mazoezi kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vyema kwenye mechi zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Badru alisema hatua ya kwanza ni kuhakikisha anapata pointi tatu katika kila mechi na 'hesabu' zake zitaanzia katika michezo minne ya viporo aliyonayo.

Badru alisema ana nafasi ya kupata ushindi zaidi kwenye mechi hizo ambazo zitakuwa ugenini na dhidi ya Namungo FC, KMC FC, Coastal Union pamoja na Yanga.

"Nilipokabidhiwa timu ilikuwa nafasi ya 15 ikiwa na pointi 15, hivyo katika mechi tano nimefanikiwa kupata pointi nane, kwa sasa nina badilisha mbinu kuhakikisha haturuhusu kufungwa tena, tunahitaji kushinda mechi zetu nne za viporo ili kutoka kwenye nafasi ya 11 na kupanda juu,".

"Kwa maandalizi yetu nina imani kubwa katika mechi hizo za viporo, kwangu ni rahisi kupata matokeo mazuri ugenini kulingana na mbinu ambazo nawapa wachezaji wangu," alisema Badru.

Aliongeza baada ya kuondolewa katika michuano ya Kombe la FA, wanahitaji kupambana ili kufikia malengo ya kumaliza kwenye nafasi tano za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ukiangalia aliyekuwa juu yetu pointi zinalingana hata aliyekuwa chini yetu pia, sasa tunahitaji kushinda mechi zetu bila kujali tunacheza nyumbani au ugenini," alisema Badru.

# Tanzania ufukweni yaipania Burundi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni, Boniface Pawasa, amesema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), dhidi ya Burundi itakayochezwa keshokutwa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Pawasa, alisema kwa sasa kikosi chake kinaendelea kujiimarisha na mazoezi na anashukuru hana mchezaji majeruhi hata mmoja.

Pawasa alisema kila mchezaji wa timu hiyo yuko tayari kupambana kuhakikisha wanapeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo.

Naye Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, alisema ana imani kikosi hicho kitafanya vizuri katika michezo yote miwili ambayo itachezwa hapa nchini.

"Jinsi ambavyo timu hii inafanya vizuri katika mazoezi ni ishara kubwa kwamba tunaweza kufanya vizuri katika mechi yetu ya kwanza dhidi ya Burundi na hatimaye kusonga mbele," alisema Kasongo.

Burundi imeomba kutumia ufukwe za Coco jijini katika mechi yake ya nyumbani na mchezo wa marudiano utachezwa hapo hapo Aprili Mosi, mwaka huu ambapo Tanzania watakuwa wenyeji.

# Namungo kamili kuikabili Nkana

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Namungo FC ambayo inashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Khamis Fakhi, amesema timu yao imejipanga vizuri kuwakabili wapinzani wao Nkana FC kutoka Zambia na wamefunga hesabu ya mechi zilizopita.

Namungo yenye makazi yake mkoani Lindi itawakaribisha Nkana FC katika mechi ya hatua ya makundi itakayochezwa Aprili 4, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Fakhi aliliambia gazeti hili kikosi chao kimejipanga vyema baada ya kufanyia kazi upungufu uliokuwa nayo na kuwaambia Watanzania wasikatishwe tamaa na matokeo yaliyopita.

"Tumejipanga vizuri kukutana na wapinzani wetu, tumewafuatilia kwa muda mrefu kipindi walipokutana na Pryramids,"alisema Fakhi.

Aliongeza wameshafahamu ubora na upungufu wa wapinzani wao hivyo wataingia uwanjani kwa tahadhari ili wasipoteze mchezo huo.

Michezo
Jumapili Machi 28, 2021
Nipashe



Ramos ashauriwa kustaafia Madrid

HABARI UK 22

## Stars, Libya kujiliwaza leo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupoteza nafasi ya kushiriki katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) itawakaribisha wenzao kutoka Libya katika mechi ya mwisho ya Kundi J itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Huku Libya pia imekosa nafasi ya kushiriki fainali hizo zitakazofanyika nchini Cameroon mwakani, Stars itashuka dimbani kusaka ushindi ili kulinda heshima ya kumpoteza aliyekuwa shabiki namba moja, Hayati Dk. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Tanzania, ambaye alifariki Machi 17, mwaka huu jijini na juzi alizikwa nyumbani kwao Chato, mkoani Geita.

Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Selemani Matola alisema waliingia uwanjani kwenye mechi ya Equatorial Guinea kwa ajili ya kupata ushindi, lakini vijana walishindwa kutumia nafasi chache zilizopatikana, lakini kwenye mechi ya mwisho wanaahidi kufanya vizuri.

"Nafahamu Watanzania wameumia sana baada ya matokeo haya, lakini tulipambana sana hadi dakika za mwisho, haikuwa matarajio yetu, nguvu zetu sasa tunazielekeza kwenye mechi yetu na Libya, kikubwa kwenye mechi hii tunacheza nyumbani na tunataka kulinda heshima," alisema Matola.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Nchini, Clifford Ndimbo, alisema maandalizi yote kuelekea mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni yamekamilika na akasisitiza itafanyika bila ya mashabiki.

Tunisia yenye pointi 13 na Equatorial Guinea yenye pointi tisa ndio zimepata tiketi ya kushiriki AFCON wakati Taifa Stars inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne huku Libya ambao wamekusanya pointi tatu wanaburuza mkia katika kundi hilo.

Ndoto ya Watanzania kucheza AFCON kwa mara ya pili mfululizo ilitoweka Alhamisi iliyopita baada ya Stars kuchapwa bao 1-0 na wenyeji Equatorial Guinea huku Libya ikiambulia kipigo cha mabao 5-2 kutoka kwa Tunisia siku hiyo.



Beki wa Azam FC, Abdalllah Kheri (kushoto) akimdhibiti beki mwenzake wa timu hiyo, Bruce Kangwa, ambaye ni raia wa Zimbabwe katika mazoezi ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA yanayotarajiwa kuendelea tena baadaye mwezi ujao. **PICHA: MTANDAO**.

# YANGA YATAMBA KUKWEPA VIUNZI

## Mwambusi asema kikosi chake kiko tayari, imara kukamilisha majukumu...

**Na Mwandishi Wetu**

TUKO tayari! Hayo ni maneno ya Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi kuelekea hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mechi za mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la FA ambazo huchezwa kwa mtindo wa mtoano.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Mwambusi alisema mazoezi ambayo amewapa wachezaji wake yamewabadilisha na kuwafanya wawe imara na tayari kwa mapambano huku akizingatia ushindani katika michezo iliyobakia ya mashindano yote wanayoshiriki.

Mwambusi alisema kila mchezaji anaonyesha 'kiu' ya kupata nafasi ya kupambana ili kufikia malengo na anaamini dhamira waliyonayo wataitekeleza kikamilifu ndani ya msimu huu wa 2020/21.

"Naweza kusema tuko tayari kwa ajili ya mapambano, tumekuwa na muda mzuri wa kufanya maandalizi kwa ajili ya mechi zijazo, ninaamini kila kitu kitakwenda vyema, kila mchezaji anafahamu vizuri majukumu yake, ligi ilisimama lakini hii yote ni mipango ya Mungu, mapumziko yametusaidia," alisema Mwambusi.

Kocha huyo alisema wachezaji wanahitaji kutwaa ubingwa ili kujihakikishia tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani na hili linawaongezea hamasa ya kutaka kufanya vizuri katika kila mechi.

"Tumeweka mikakati ya ushindi, kila mechi kwetu ni fainali, tunataka kila mchezo uwe na matokeo mazuri, tusiangalie mbele, tumalize mechi moja baada ya nyingine, kwetu mechi zote ni muhimu na hatutaidharau klabu yoyote," aliongeza kocha huyo.

Alisema programu ya mazoezi ya 'gym' ambayo wameianza hivi karibuni imewabadilisha wachezaji wake na kuwaongezea nguvu ya kupambana.

"Kuna vitu walikuwa hawafanyi, sasa hivi tunavifanya, najua tuko kwenye vita ya kuwania ubingwa, ni lazima ujiimarishe kwa kutumia mbinu zote, hatutaki kuwapa nafasi wapinzani, tutaingia kumaliza msimu kwa kasi, tunataka kurejesha furaha iliyopotea kwa miaka mitatu," alisema Mwambusi.

Kuhusu nyota wake ambao wako kwenye timu za taifa mbalimbali, Mwambusi alisema anaamini kila mmoja anajituma katika mazoezi ili kulinda viwango vyao na watakaporejea atawaandalia pia programu maalumu ili kuwaweka sawa.

"Naamini itatuchukua siku chache kutengeneza muunganiko, kwa sababu wote wako kwenye mazoezi, haitakuwa tatizo, watafikia katika kiwango ninachokihitaji, wamekwenda kwenye klabu za mpira, mazoezi yanafanana, vitu vichache hutofautiana na ni kwa sababu ya kutengeneza mfumo," Mwambusi aliongeza.

Kikosi cha Yanga kimeweka kambi yake katika Kijiji cha Avic Town, kilichoko eneo la Kigamboni nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Yanga yenye pointi 50 ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 46, lakini wamecheza mechi tatu pungufu huku Mwadui FC ya mkoani Shinyanga iliyojikusanyia pointi 16 ikiburuza mkia.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042